**30 AGOSTI, 2023**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MBILI

### Kikao cha Pili – Tarehe 30 Agosti, 2023

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA - KATIBU MEZANI:**

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):**

Maelezo ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi juu ya Azimio la Bunge kuhusu Mapendekezo ya Kuridhia Katiba ya Tume ya Usafiri wa Anga ya Afrika ya Mwaka 2009 *(The Constitution of the African Civil Aviation Commission, 2009)*.

**MHE. GHATI Z. CHOMETE K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu juu ya Azimio la Bunge kuhusu Mapendekezo ya Kuridhia Katiba ya Tume ya Usafiri wa Anga ya Afrika ya Mwaka 2009 (*The Constitution of the African Civil Aviation Commission, 2009)*.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Maswali tunaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Mwantumu Zodo.

Na. 21

### Ujenzi wa stendi ya mabasi ya kisasa – Tanga

**MHE. MWANTUMU M. ZODO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga stendi za mabasi katika Halmashauri za Mkoa wa Tanga?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwantumu Mzamili Zodo, Mbunge Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia mpando wa uboreshaji wa Majiji na Manispaa Tanzania *TSCP* imejenga Stendi ya Kisasa katika Jiji la Tanga na Halmashauri ya Mji wa Korogwe zilizogharimu takribani kiasi cha Shilingi billioni 10.7, ujenzi wa stendi hizo umekamilika na zinatumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika mwaka wa fedha wa 2023/2024 Serikali imetenga bajeti ya shilingi billioni 10.312 kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu ya stendi katika halmashauri nchini. Aidha, Serikali itaendelea kujenga stendi za mabasi katika halmashauri kwa awamu kupitia programu mbalimbali kama, *TACTIC*, *TSCP* na vyanzo vingine yakiwemo mapato ya ndani ya halmashauri, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zodo.

**MHE. MWANTUMU M. ZODO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Miradi hiyo iliyotajwa hapo ni kwa ajili ya uboreshaji wa stendi za majiji na manispaa na kwa kuwa halmashauri ninazoziongelea haziangukii kwenye majiji wala manispaa. Je, Serikali inampango gani wa makusudi sasa kuhakikisha wanakwenda kuboresha stendi kwenye Halmashauri zetu za Wilaya ya Mkinga, Pangani, Muheza, Lushoto pamoja na Kilindi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa maeneo ya stendi pia ni moja ya chanzo cha uzalishaji wa ajira hasa kwa kina mama na vijana. Je, Serikali sasa ina mkakati gani wa kuhakikisha miundombinu ya stendi inakuwa rafiki kwa wajasiliamali? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mwantumu Mzamili Zodo, Mbunge wa viti maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, halmashauri ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja ni kweli hazipo kwenye *category* ya majiji na manispaa na halmashauri hizi kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi, kwamba tutaendelea kutenga fedha kupitia mapato ya ndani lakini pia kupitia Serikali kuu kwa awamu kuhakikisha kwamba stendi hizo zinajengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba halmashauri hizo pia zipo kwenye mpango, tutaendelea kujenga kwa awamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili kuhusiana na miundombinu inayowezesha wafanya biashara. Serikali imekuwa ikijenga stendi, inajenga maeneo kwa ajili ya mama lishe na baba lishe, inajenga maeneo ambayo yanaweza ku–*accomodate* Machinga na wafanyabiashara wadogowadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo suala hili litaendelea kutekelezwa, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Innocent Bilakwate.

Na. 22

**Uhitaji wa ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Songambele – Kyerwa**

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Afya katika Kata ya Songambele ili kupunguza msongamano kwenye Kituo cha Afya Nkwenda Wilayani Kyerwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, Mbunge wa Jimbo la Kyerwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2021/2022, Serikali ilitenga bajeti ya shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Rutunguru katika Tarafa ya Kaisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya ujenzi wa Vituo vya Afya kwenye Kata za kimkakati kote nchini ikiwemo Kata ya Songambele iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bilakwate.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, swali langu la kwanza, kwenye Wilaya ya Kyerwa tunayo maboma ambayo yanazidi ya miaka 10 mpaka 15. Kwa mfano Kata ya Kimuli kuna boma ambalo linazaidi ya miaka 15 halijakamilishwa na ni nguvu ya wananchi. Kata ya Kikukuru kuna Zahanati ya Omkutembe na yenyewe haijakamilika zaidi ya miaka 10. Je, ni lini Serikali itakamilisha maboma haya ili wananchi waweze kupata huduma? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Niabu, Spika ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Bilakwate, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kutoa fedha kwa ajili ya ukamililishaji wa maboma ambayo yameanza kujengwa kwa nguvu za wananchi nchini kote na mpaka mwezi Juni mwaka huu jumla maboma elfu moja na sitini na sita Serikali ilikuwa imepeleka fedha yamekamilishwa ujenzi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi hili linaendelea kwa awamu. Kwa hiyo, ni mhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba maboma haya ya zahanati yenye umri mrefu wa miaka 10 na zaidi yatapewa kipaumbele kwenye bajeti za Serikali. Pia naelekeza kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, kwamba Halmashauri hii ya kyerwa watenge pia mapato ya ndani kuhakikisha wanakamilisha majengo haya kwa huduma za wananchi, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Midimu.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Kituo cha Afya Kiloleni Wilaya ya Busega hakina wodi za kulaza wagonjwa, wodi ya wanaume, wanawake na watoto. Je, ni lini Serikali itajenga wodi hizo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther Midimu, Mbunge wa viti maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kituo cha Afya cha Kiloleni katika Halmashauri ya Busega hakina wodi za kulaza wagonjwa. Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, kwamba vituo hivi vya afya vinajengwa kwa awamu. Tunaanza na awamu ya kwanza ya majengo ya *OPD*, Maabara lakini pia majengo ya mama na mtoto na majengo ya upasuaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua zinazofuata ni kukamilisha kujenga mawodi na miundombinu mingine. Kwa hiyo, ni mhakikishie Mheshimiwa Mbunge, muda huo utakapofika tutahakikisha pia tunatafuta fedha kwa ajili ya kituo hiki cha afya cha Kiloleni, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Suma.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Halmashauri ya Busekelo wananchi wamejenga maboma kwa ajili ya vituo vya afya, maboma manne. Ikiwa ni Kata ya Lufilyo, Kisegese, Mpombo na Kambasegela. Je, ni lini Serikali itaunga juhudi za wananchi hao kukamilisha maboma hayo ya vituo vya afya? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Suma Fyandomo, Mbunge wa viti maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niwapongeze wananchi wa Jimbo la Busekelo kwa kutoa nguvu zao kuanzisha ujenzi wa maboma ya vituo vya afya, lakini niwahakikishie tu kwamba, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kukamilisha vituo vya afya kwenye kata za kimkakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakwenda kufanya tathimini kuona kati ya hayo maboma lipi ni lakimkakati ili Serikali itafute fedha kwa ajili ya kuwaunga mkono kukamilisha maboma hayo, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aida.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Serikali ilitoa fedha kwa ajili ya kujenga Kituo cha Afya cha Kabwe, lakini mpaka leo kile kituo hakijakamilika kwa sababu fedha hazitoshi. Ni mkakati upi wa Serikali wa kumalizia kituo kile cha afya ili wananchi wa Kabwe wapate huduma pamoja na kata ya jirani ya Korongwe? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Aida Khenani, Mbunge wa Jimbo la Nkasi Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kituo cha afya cha Kabwe kilipelekewa fedha na Serikali kwa ajili ya ujenzi na kwa taarifa kwamba hakijakamilika tutakwenda kwanza kujifunza kwa nini fedha iliyopelekwa haijakamilisha majengo. Kama kuna matumizi mabaya ya fedha ya Serikali wanaohusika watakaothibitika tutachukua hatua za kisheria na za kinidhamu. Lakini pia tutatafuta pia fedha kuhakikisha kwamba kituo kinakamilika na kuanza kutoa huduma kwa wananchi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Abasi Tarimba, kwa niaba ya Mheshimiwa Kisangi.

Na. 23

**Kuondolewa sharti la kukopa kwa vikundi – mikopo ya Halmashauri**

**MHE. MARIAM N. KISANGI K.n.y. MHE. TARIMBA G. ABBAS** aliuliza:-

Je, Serikali haioni sasa ni wakati wa kuondoa sharti la kukopa kwa vikundi mikopo inayotolewa na Halmashauri?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, Mbunge wa Jimbo la Kinondoni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeunda Timu ya Kitaifa kwa lengo la kupitia na kutoa mapendekezo ya namna bora ya kuratibu na kusimamia utoaji wa mikopo ya asilimia 10 kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Timu hiyo imekalimisha jukumu hilo na kukabidhi taarifa Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali inaendelea na uchambuzi na mapitio ya taarifa na pindi itakapokamilika taarifa rasmi itatolewa kwa Umma juu ya utaratibu wa mikopo ya asilimia 10 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kisangi.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninayo maswali ya nyongeza. Kwa kuwa changamoto ya mikopo ya vikundi imekuwa kubwa sana katika maeneo ya Jiji la Dar es salaam na hususani katika Jimbo la Kinondoni, kutokana na masharti mbalimbali wanayopewa wakopaji wanashindwa kukopa. Je, Serikali haioni haja katika hiyo mikakati yake sasa kuangalia sehemu ya mtu kukopa mmoja mmoja?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa wakinamama wengi wajasiliamali wa mitaani wanashindwa kuungana kwenye vikundi na wanahitaji kupata mikopo mmoja mmoja mwenye kuuza mandazi, vitumbua na nini. Je, Serikali imejipanga vipi sasa katika hiyo mikakati yake kuhakikisha kwamba, sasa wanaruhusiwa kukopa mtu mmoja mmoja ili aendeleze biashara yake? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri kwa KIfupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mariam Kisangi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ifahamike kwamba vikundi katika mikopo ya asilimia 10 vinatumika kama dhamana, kwa sababu wajasiliamali wanaokopeshwa kwa mikopo ya asilimia 10 ni wale ambao hawana uwezo wa kutosha kuwa na dhamana ya kupewa mkopo. Kwa hiyo, *concept* ilikuwa kwamba kikundi ni dhamana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme tumechukua hoja hii na chini ya Mheshimiwa Waziri wetu wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, tutaifanyia tathimini kwenye tathimini inayoendelea nakuona uwezekano wakuiboresha kama itakuwa inatija, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ndaisaba, jiandae. Mheshimiwa Jerry Silaa.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, wewe si uliomba kuchukua kwa niaba hili swali?

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimeomba...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jerry Silaa.

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Vijana wengi wa Dar es salaam wanaendesha bodaboda za mikataba. Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka kushirikiana na ma-*bank* yanayotoa mikopo ya bodaboda *bank* ya *NMB* na *bank* ya *CRDB* ili wanapofungua sasa dirisha la mikopo hii ya asilimia 4:4:2 za vijana, wanawake waweze kutoa mikopo ya vijana kuwakwamua kwenye unyonyaji wa mikataba hii ya bodaboda? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba arudie sijalielewa swali lake.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jerry, rudia tena.

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wengi wanaoendesha bodaboda, wanapewa mikataba na matajiri na wanatumika kwa muda mrefu kurejesha pesa na kwa kufanya hivyo wanaonyesha uwezo wao wa kurejesha mikopo.

Je, Serikali haioni kwenye mpango mpya wa kutoa mikopo hii washirikiane na ma-*bank* yanayotoa mikopo ya bodaboda kwa kutoa fedha zile za *seed money* ili vijana wengi wapate mikopo ya bodaboda waweze kujikwamua kwenye unyonyaji wa mikataba ya matajiri? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jerry Silaa, Mbunge wa Jimbo la Ukonga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema utaratibu wa ukopeshaji wa asilimia 10 unafanyiwa kazi na utaboreshwa, kwa hivyo tutaona pia uwezekano wakuchukua wazo hili na kuliboresha kuona namna ambavyo utawezesha vijana kupata mikopo kwa urahisi zaidi kwa kadri ambavyo itaonekana inawezekana, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Dau.

Na. 24

**Kudhibiti vyombo vinavyozidisha mizigo na abiria baharini**

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kudhibiti vyombo vya baharini vinavyozidisha mizigo na abiria?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwantum Dau Haji, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vyombo vikubwa ikiwa ni vyombo vyenye urefu zaidi ya mita ishirini na nne. Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania *TASAC* linajukumu kisheria kufanya ukaguzi wa michoro ya meli kabla ya hatua ya ujenzi kuhakikisha mstari wa ujazo *(load line)* umewekwa kwenye kina sahihi cha meli, kisha Msajili wa meli anathibitisha michoro hiyo na kutoa ruhusa ya ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, *TASAC* kufanya ukaguzi kipindi cha ujenzi wa meli. *TASAC* hufanya Ukaguzi kuhakikisha Meli inapakia mizigo bila kupitiliza mstari wa ujazo uliothibitishwa na Msajili, na endapo itabainika kuwa meli imezidisha ujazo wa abiria, mizigo au vyote kwa pamoja itakuwa imetenda kosa kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, meli hiyo itapaswa kuzuiliwa bandarini na Mamlaka ya Bandari Tanzania itajulishwa ili kusitisha kutoa kibali kwa meli hiyo hapo bandarini. Kwa hatua zaidi, *TASAC* humtoza mmiliki au nahodha wa meli faini na kisha kusimamia upunguzwaji wa abiria, mizigo na vyote kwa pamoja kisha kuruhusu

meli hiyo pindi Mkaguzi atakapojiridhisha kuwa Meli ipo salama kwa kuanza safari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa vyombo vidogo vyenye urefu chini ya mita ishirini na nne, *TASAC* inajukumu kisheria kufanya ukaguzi wa vyombo vidogo na kutoa leseni ya uendeshaji inavyotaka ujazo wa abiria au mizigo unaostahili kuzingatiwa katika uendeshaji wa chombo.

Mheshimiwa Naibu Spika, endapo itabainika kuwa chombo kimezidisha ujazo wa abiria au mizigo, nahodha atakuwa ametenda kosa kisheria na chombo hicho kitazuiliwa bandarini au mwaloni ili kulipa faini na *TASAC* kusimamia upunguzwaji wa abiria au mizigo kabla ya kuruhusu chombo kuendelea na safari, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dau.

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ambayo ameegemea zaidi kwenye mtazamo wa Sheria badala ya hali halisi ilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo maswali mawili ya nyongeza. Je, ni lini mmechukua hatua kwa meli zilizozidisha abiria na kusababisha vifo vingi zaidi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania inavyombo vingapi? Vinavyotoa huduma za abiria na mizigo baharini na maziwa makuu? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE)**: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, Mwantumu Dau Haji, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kuna baadhi ya vyombo huwa vinakiuka sheria kwa kuzidisha uzito wa abiria na mizigo. Kupitia *TASAC* tunatoa elimu kwa wamiliki wa vyombo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spaka, pili; sheria inatutaka kwa yeyote atakayezidisha uzito kulipa faini na kabla meli haijaondoka kuna Maafisa ambao wanahakikisha mstari wa ujazo haujazidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, faini hizo zinatofautiana kulingana na urefu wa chombo na chombo. Chombo chenye urefu wa mita zaidi ya 24 wanalipa faini ya shilingi laki nne na chombo chenye urefu chini ya mita 24 wanalipa faini ya shilingi laki mbili lakini ikithibitika pia huyo mmiliki ameshindwa kulipa faini hiyo anapelekwa Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili ameuliza idadi ya vyombo tulivyonavyo hapa nchini. Kwa Sensa ambayo ilifanywa na *TASAC* mwaka 2021 kwa kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu wa Taifa *(NBS)* inaonesha vyombo vyote tulivyonavyo hapa nchini kwa ukanda wa bahari, maziwa makuu yote, mito na maziwa madogo ni 52,189; hii ndiyo takwimu iliyofanyika mwaka 2021. Na kati ya vyombo hivyo asilimia 53.6 vipo Ziwa Victoria, asilimia 13.4 vipo Bahari ya Hindi, asilimia 10.2 vipo Ziwa Tanganyika, asilimia 7.6 vipo Ziwa Nyasa na asilimia 15.2 vipo maeneo ya Maziwa Madogo pamoja na Mito. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Mwambe.

Na**.** 25

**Malipo ya fidia kwa wananchi wa Nanganga - Ndanda**

**MHE. CECIL D. MWAMBE** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali italipa fidia eneo la Nanganga ambako ujenzi wa barabara iendayo Ruangwa unaendelea?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cecil David Mwambe, Mbunge wa Ndanda, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Barabara Na. 13 ya Mwaka 2007 na Kanuni zake za Mwaka 2009 wananchi ambao mali zao zipo ndani ya mita 22.5 hawatastahili kulipwa fidia kwani wamo ndani ya eneo la hifadhi ya barabara. Kwa upande wa wananchi ambao wamo ndani ya nyongeza za mita 7.5 kwa nchi nzima Serikali inafanya kazi na kuandaa mapendekezo ambayo yatabainisha maeneo gani wananchi wataruhusiwa kuyaendeleza na yapi Serikali itayachukua na kuyalipa fidia. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwambe.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza sikubaliani na majibu yaliyotolewa na Serikali na swali hili limerudi kwa mara ya pili baada ya maelekezo ya Mheshimiwa Spika wakati fulani hapo nyuma kwa sababu zifuatazo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili tunalolizungumzia barabara ilihama kwenye *original plan* na barabara hii imewafuata wananchi. Kwa sababu hiyo haina *qualification* ya mita 22 wala mita hizo zinazotajwa 22.5 wala nyongeza ya mita 7.5. Mheshimiwa Waziri Mbarawa alifika kwenye hiki kijiji tarehe 22 mwezi wa kwanza, mwaka 2022 eneo ambalo Misikiti, Kanisa pamoja na Nyumba za Serikali zilivunjwa. Swali langu la msingi ni lini Serikali itakwenda kulipa fidia kwa sababu wenyewe walifuatwa na barabara na si wao waliifuata barabara? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi; kwamba

kama barabara imemfuata mwananchi ama imehama na kwenda sehemu ambayo haikuwepo maana yake hawa watu wanastahili fidia; na kama suala alilolielezea Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara imehama kabisa. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba wananchi hawa watakuwa wanastahili fidia. Kwa hiyo, kwa sababu swali lake ni *specific* na eneo linalohusika, naomba baada ya hapa tuweze kukutana naye ili tuweze kuangalia. Kama barabara iliwafuata hawa wananchi kama alivyosema basi wananchi hao wana haki ya kulipwa fidia. Ahsante.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza;

Je, ni lini Serikali itawalipa fidia wananchi waliopisha Barabara ya Mianzini – Sambasha - Kimyaki hadi Ngaramtoni?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama Ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli barabara hii ni mpya na imefunguliwa. Tayari tulishandaa taratibu za kuwalipa wananchi ambao tumeifungua ile barabara, na barabara iliyoanza ni mpya wananchi hao watalipwa mara baada ya kukamilisha taratibu zote za fidia, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hokororo.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa tangu tathmini ya malipo ya fidia kwa wananchi wa Nanganga yamefanyika muda mrefu umepita.

Je, Serikali iko tayari kuongeza kiwango cha fidia kwa wananchi wale kwa sababu walisimama kabisa katika maendeleo yao? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni utaratibu wa Serikali kwamba kama fidia imefanyiwa tathmini ikapita miezi sita ni lazima turudi kuhuisha tena ile tathmini ili kupata thamani ya wakati huo. Kwa hiyo itafanyiwa tathmini mpya kama imepita miezi sita na watalipwa sasa fidia ya wakati huu, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA**: Ahsante. Mheshimiwa Oran.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Napenda kuuliza barabara ya *Bypass* ya Uyole – Songwe, ni lini wananchi watalipwa fidia waliopisha hiyo barabara ya *by pass?*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE.ENG GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara inayotajwa ndiyo kwanza wakandarasi wameshakabidhiwa, na ipo kwenye huu mpamgo wa *EPC+F*. Jana nilijibu kwamba moja ya vitu ambavyo sasa hivi vinafanyika ni kupitia upya na kufanya tathmini ya malipo yatakayofanyika kwa ajili ya wale wananchi ambao watapisha, ikiwa ni pamoja na wananchi wa hiyo Barabara ya Uyole – Songwe *Bypass*. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Michael.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Barabara ya Makofia- Mlandizi – Mzenga mpaka Vikumbulu miaka mitatu iliyopita walifanyiwa tathmini ya kilomita 30 na miezi miwili iliyopita wamerudi kubadilisha kurudi kwenye mita 22.5;

Je, ni lini wananchi wale watalipwa fidia pamoja na mabadilko hayo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, tayari tumekwenda kwa ajili ya kufanya tathmini kwa watu ambao wapo ndani ya mita 22.5. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba maandalizi yanafanyika ndiyo maana tumekwenda sasa hivi ili waweze kulipwa fidia. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Seif kwa niaba yake, Mheshimiwa Venant.

Na. 26

**Ujenzi wa barabara ya Choma – Puge**

**MHE. VENANT D. PROTAS K.n.y. MHE. SEIF K. S. GULAMALI** aliuliza: -

Je, ni lini ujenzi wa barabara ya Choma - Ziba – Nkinga - Simbo - Puge utaanza kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Seif Khamis Said Gulamali, Mbunge wa Manonga kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* tayari imeanza maandalizi kwa ajili ya ujenzi wa kiwango cha lami kwa barabara ya Choma – Ziba – Nkinga – Simbo – Puge yenye urefu wa kilometa 109 ambapo Mhandisi Mshauri kwa ajili ya kufanya kazi ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina amepatikana na ameanza kazi tarehe 24 Agosti, 2023 na anatarajia kukamilisha mwishoni mwa mwezi Oktoba, 2024. Baada

ya kazi ya usanifu kukamilika, Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Venant.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na majibu mazuri ya Waziri barabara hii ipo kwenye Ilani ya Uchaguzi ya 2020/2025 na huenda pia kwenye Bajeti iliyopita Waziri aliliahidi Bunge hili kuwa atatenga fedha kwenda kuanza usanifu katika barabara hii;

Je, ni lini Serikali itapeleka fedha ili wananchi hao waanze kufanyiwa usanifu ili barabara yao ijengwe?

Mheshimwa Naibu Spika, swali langu la pili, barabara ya Chaya – Nyaua, Chanya – Manyoni – Tabora yenye kilomita zaidi ya 200, sasa kumekuwa na msongamano wa magari mengi. Tuliomba pendekezo la kuiweka *bypass* ya Kigwa – Magili;

Je, ni lini Serikali itaanza usanifu wa kuiweka barabara ya Kigwa- Magili ili iweze kupata kiwango cha lami? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika kama nilivyosema, barabara hii ya Chimo – Simbo hadi Puge ilikuwa haijafanyiwa usanifu; na tayari tumeshaanza kufanya usanifu. Wakati wa Bajeti ni kweli Waziri aliahidi kwamba tutaanza kujenga kilomita 10 kwa kiwango cha lami, lakini kilomita hizi zitaanza kujengwa pale tu ambapo usanifu utakuwa umekamilika, hizo kilomita za awali kilomita 10. Barabara ya pili Serikali inaendelea kutafuta fedha ili iweze kujengwa kwa kiwango cha lami kama alivyoomba Mheshimiwa Mbunge. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mabula.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumuuliza swali Mheshimiwa Naibu Waziri. Barabara ya Kenyatta itokayo Mwanza Mjini kwenda Shinyanga ambayo tayari imeshafanyiwa upembuzi yakinifu na umeshakamilika, pia usanifu umekamilika. Barabara imezidi kuwa na msongamano mkubwa;

Je, ni lini sasa Serikali itahakikisha barabara hii inapanuliwa kwa njia nne? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE),** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli moja ya barabara katika majiji ambayo sasa hivi ina magari mengi ni hiyo Barabara ya Kenyatta kwenda Usagara kuelekea Shinyanga. Serikali imeshafanya usanifu na sasa hivi inatafuta fedha kwa ajili ya kuijenga barabara hiyo kwa njia nne ili kupunguza changamoto kubwa ya foleni katika Jiji la Mwanza, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bupe.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Je, ni lini Serikali itajenga barabara ya kutoka Kaoze- Chombe kwenda Igonda iliyopo Sumbawanga Vijijini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE.ENG. GODFREY K. MSONGWE**): Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii bado hatujaiingiza kwenye mpango wa kuijenga kwa mwaka huu. Lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kabla ya kuanza kuijenga tutatafuta fedha kwa ajili ya kuifanyia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina katika bajeti inayokuja, siyo kwa bajeti hii; kwamba hatukuipangia fedha kwa ajili ya kuijenga kwa kiwango cha lami.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Nyamoga.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Ni lini mkandarasi wa kujenga Barabara ya kutoka Iringa Mjini kwenda Kilolo ataweka saini mkataba na kuanza ujenzi? Kwa sababu limekuwa ni jambo la muda mrefu na wananchi wanasubiri kwa hamu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hii kwanza inafadhiliwa na *World Bank,* na fedha zipo. Kinachoendelea sasa hivi ni kukamilisha tu taratibu kati ya Serikali na mkandarasi ambaye tayari alishapatikana ili aweze kukabidhiwa hiyo *site* kujenga hizo kilomita 33 za Iringa kwenda Kilolo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Tunaendelea. Wizara ya Afya, Mheshimiwa Kyombo.

Na. 27

**Kufutwa kwa *Form 2C* katika huduma ya Bima**

**MHE. FLORENT L. KYOMBO** aliuliza: -

Je, Serikali haioni kuwa kufutwa kwa *Form 2c* katika huduma ya Bima ya Afya inakosesha mgonjwa kupata dawa iliyokosekana hospitali aliyotibiwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT FESTO J. DUGANGE) K.n.y. WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Mbunge wa Nkenge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, maamuzi ya Serikali ya kusitisha matumizi ya fomu za dawa *(Form 2C)* katika vituo vya kutolea huduma za afya yalifanyika kwa kuzingatia manufaa yake, ikiwemo utekelezaji wa maelekezo ya watoa huduma wote wa Serikali. Kwamba kuwe na utaratibu wa kuanzisha maduka ya dawa yanayomilikiwa na hospitali na hivyo kuongeza mapato ya ndani ya hospitali. Pia kuepusha usumbufu kwa wananchi wa kutafuta dawa nje ya hospitali na hivyo kusabisha lawama zisizo za lazima kwa Serikali. Vilevile na kuepusha vitendo vya udanganyifu vinavyofanywa katika eneo la dawa dhidi ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Wizara imevielekeza vituo vya kutolea huduma kuweka utaratibu wa Mgonjwa kupata dawa iliyokosekana hospitali aliyotibiwa ili kuepusha usumbufu kwa wananchi. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kyombo.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa maelezo mazuri ya Serikali na niipongeze Serikali kwa kweli dawa zipo kwenye vituo vyetu na wananchi wanapata dawa. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, ni nini mkakati madhubuti wa Serikali kuhakikisha kuwa dawa hizi zinazopatikana sasa hivi ziendelee kupatikana katika vituo vya afya?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, tupate ufafanuzi wa utaratibu uliowekwa pale mgonjwa anapokosa dawa katika hospitali na duka linalomilikiwa na hospitali ili sasa apate dawa kwa ajili ya tiba inayohusiana na matibabu yake, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT FESTO J. DUGANGE) K.n.y. WAZIRI WA AFYA:**

Mhehimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mkakati wa kuhakikisha kwamba baadhi ya dawa ambazo zinakosekana zinapatikana, moja, tumeelekeza na kusisitiza vituo vyote vya Serikali vifungue maduka ya dawa. Mbali na *dispensing* za hospitali zenyewe lakini wafungue maduka ya dawa ndani ya hospitali zenyewe, na wahakikishe yale maduka yana dawa zote zilizopo katika ngazi ya kituo husika; ili mgonjwa akikosa dawa pale *dispensing* aweze kuwa-*referred* ndani ya hospitali kwenda kuchukua dawa kwenye duka la dawa la hospitali. Kwenye mkakati huo tumeweka kwamba dawa zote lazima zipatikane kwenye duka, ikiwa ni *alternative* ya *filling* kutoka *dispensing*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, utaratibu ni kwamba mara mgonjwa akiandikiwa cheti cha dawa na kwenda dirisha la dawa kupata dawa zile akapata chache na moja kakosa anaandikiwa cheti kidogo kwa ajili ya kwenda kwenye duka la dawa na kupata dawa zile; na tutaendelea kusimamia utaratibu huo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Wizara ya Mawasiliano, Mheshimiwa Mbogo.

Na. 28

**Hitaji la mawasiliano eneo la Sikonge hadi Inyonga**

**MHE. TASKA R. MBOGO,** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Mkongo wa Mawasiliano katika eneo la Sikonge hadi Inyonga?

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI,** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi na uendelezaji wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kwa kuwa ni muhimili wa mawasiliano hapa nchini. Katika mwaka huu wa fedha 2023/2024 Serikali imepanga kujenga Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kuanzia Tabora – Sikonge – Inyonga – Majimoto – Kizi wenye urefu wa Kilomita 369.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hadi sasa Serikali kupitia Shirika la Mawasiliano Tanzania *(TTCL)* imesaini mkataba na Mkandarasi kwa ajili ya kujenga Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano katika maeneo hayo. Hatua za utekelezaji zimeanza ambapo unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Juni, 2024.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Taska.

**MHE. TASKA R. MBOGO :** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali ninayo maswali mawili ya nyongeza. Kwanza naipongeza serikali kwa kutufikiria kujenga Mkongo wa Taifa kutoka Sikonge mpaka Inyonga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutoka Sikonge, Ipole, Inyonga mpaka Mpanda hakuna mawasiliano, Mkongo wa Taifa unaoenda kujengwa unatoka Inyonga kwenda Majimoto mpaka Kizi. Kutoka Inyonga kwenda Mpanda kuna kilomita 130, hapana mawasiliano na ni hifadhi ya Taifa;

Je, Serikali ina mkakati gani wa kujenga Mkongo wa Taifa katika eneo hilo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kwenye Mkoa wangu wa Katavi kuna vijiji ambavyo mawasiliano ni duni. Kwa mfano Kijiji cha Bujombe Wilaya ya Tanganyika na Kijiji cha Mapili kata ya Ilela. Kuna ahadi yako Mheshimiwa Waziri ulisema utaweka Mkonga wa *Vodacom*;

Je, ni lini utatimiza ahadi yako?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Restituta Mboga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kutoka Sikonge kufauta ile barabra ya lami, sehemu kubwa ya eneo lile halina huduma ya mawasiliano. Serikali kupitia *TTCL* tumefanya tathmini na tumekusudia kuweka minara mitatu mpaka minne kwenye hilo, eneo ili hilo eneo lipate mawasiliano. Tunajua lipo tatizo kubwa la watu kusafiri hasa wakati wa usiku kwa sababu ya kukosa mawasiliano. Tumeshaweka utaratibu na tumefanya tathmini. Wakati tunajenga huu Mkongo na nguzo za mawasiliano zitawekwa kwenye haya maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule alikokutaja kwenye kijiji tunafanya tathmni upo mnara karibu na hiki kijiji tuone kama ukiongezwa nguvu tuone kama unaweza kuhudumia eneo hili. Lakini lile eneo ambalo nilitoa hadi kwmba tutaweka mnara *Vodacom* kwenye ile minara 758 kuna mnara mmoja ambao unakwenda kujengwa kwenye hili eneo. Hatua za awali za manunuzi zimekamilika vifaa vipo njiani vinakuja na ujenzi utaanza mara moja kwa ajili ya kutoa huduma kwenye eneo husika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kakunda.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Ningependa kuiuliza Serikali, wakati tunasubiri utekelezaji wa mikataba iliyosainiwa mwezi Juni, je, kuna mpango gani wa kuongeza nguvu minara ambayo ipo, ambayo ina nguvu ndogo sana inayotoa mawasiliano kwenye maeneo madogo sana?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kakunda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye bajeti iliyopitishwa hapa Bungeni ya mwaka 2023/2024, bajeti imepitishwa ya kuongeza nguvu ya minara 388 kwa ajili ya kuiongezea nguvu kama ambayo Mheshimiwa Mbunge ametoa ushauri. Naamini maeneo anayoyataja yanaweza kuwa sehemu ya hii 388 na kama hayamo, bado kuna fedha nyingine kutoka Benki ya Dunia kwa ajili ya kuongeza uwezo wa minara ambayo tunayo ili tuachane na huduma ya *2G* tuende kwenye *3G, 4G* na sasa *5G*.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea. Wizara ya Elimu, Mheshimiwa Katimba.

Na. 29

**Kuboresha Mitaala ya Elimu nchini**

**MHE. JUDITH S. KAPINGA K.n.y. MHE. ZAINAB A. KATIMBA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaboresha Mitaala ya Elimu ili mafunzo ya biashara yatolewe kuanzia shule za Msingi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zainab Athman Katimba, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iko katika hatua za ukamilishaji wa mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya 2014 na Mitaala katika ngazi ya Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Mafunzo ya Ualimu. Aidha, Wizara imevielekeza Vyuo Vikuu kuhuisha na kufanya maboresho ya mitaala yote ili iendane na Dira na Mipango

ya Maendeleo ya Taifa katika kutoa elimu itakayompa kijana wa Kitanzania ujuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inatambua umuhimu wa Somo la Biashara na hivyo somo hili limepangwa kuwa ni somo la lazima kwa wanafunzi wote kuanzia Kidato cha kwanza hadi cha nne kwa mikondo yote miwili ya elimu ya jumla na elimu ya amali. Aidha, kwa ngazi ya elimu ya msingi darasa la I - VI mitaala imetilia mkazo elimu ya fedha pamoja na elimu ya ujasiriamali ambapo elimu ya fedha imechopekwa kwenye somo la Hisabati na elimu ya ujasiriamali imechopekwa kwenye somo la sanaa na michezo, lugha, jiografia na mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyuo Vikuu vya Serikali na Binafsi kupitia Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi *(Higher Education for Economic Transformation – HEET)* vimepata mafunzo mbalimbali ya kuandaa programu zinazoendana na vipaumbele vya nchi na mahitaji ya soko la ajira. Kupitia utaratibu huu, zaidi ya programu 300 zitaanzishwa na kuhuishwa ikiwemo somo la biashara ili kuendana na mahitaji ya sasa ya kijamii, kiuchumi na soko la ajira. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Dkt. Kapinga.

**MHE. JUDITH S. KAPINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili madogo ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa dunia ya sasa ipo katika mapinduzi ya nne ya viwanda kuelekea mapinduzi ya tano ya viwanda. Je, mitaala inayoboreshwa itaendana na kasi hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; programu ya mageuzi ya kiuchumi ambayo imepelekea kuanzishwa kwa takribani programu 300 kwenye vyuo vikuu. Je, ni lini programu hizi zitahuishwa na kuanza kufundishwa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kapinga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyokwishaeleza kwenye majibu ya swali la msingi kwamba, sasa tuko katika hatua za mwisho za uboreshaji wa mitaala hii. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge katika swali lake la kwanza anazungumza kuhusiana na suala la mitaala namna gani litaweza ku-*cope* na mapinduzi ya viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, mitaala inayoboreshwa inalenga kumpatia mhitimu maarifa, *study* pamoja na ujuzi utakaomwezesha kukabiliana na mabadiliko ya kisayansi, teknolojia na kiuchumi kwa ujumla. Mitaala hii imesisitiza sana masomo ya TEHAMA pamoja na kompyuta ambayo, tutaanzia katika ngazi ya elimu ya msingi na kwenda katika ngazi zote. Lengo kuu la kufanya maboresho haya ni kujiandaa na mapinduzi haya ya nne pamoja na ya tano ya viwanda ambayo yanahusisha matumizi ya teknolojia pamoja na kompyuta kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake la pili anaulizia kuhusiana na tunaanza lini? Mradi huu wa *Higher Education for Economic Transformation* ni mradi wa miaka mitano na utekelezaji wake ulianza tokea mwaka 2021/2022 na tunatarajia kukamilisha 2025/2026. Kwa hiyo, kazi hii imeshaanza, wataalam wetu wameshapata mafunzo kwa ajili ya uboreshaji wa mitaala pamoja na programu hizi. Kazi hii inaendelea na kwa vile ni kazi ya miaka mitano, tutakuwa tunaendelea kuifanya mpaka kipindi hicho chote kitakapokuwa kimekamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Monni.

Na. 30

**Usambazaji wa umeme vijiji vya Chemba**

**MHE. MOHAMED L. MONNI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha kusambaza umeme katika Vijiji vya Chemba?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni, Mbunge wa Chemba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)* inatekeleza Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili ambapo, vijiji vyote ambavyo havina umeme Tanzania Bara vitafikiwa na huduma ya umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Chemba, Mkandarasi *M/s Sagemcom Limited* alipewa jumla ya vijiji 59 ambavyo havikuwa na umeme. Hadi kufikia tarehe 15 Agosti, 2023, vijiji 47 vimeshawashiwa umeme na vijiji 12 viko kwenye hatua mbalimbali za utekelezaji na vitakamilika kabla ya mkataba wa mkandarasi kuisha tarehe 31 Oktoba, 2023.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Monni.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Katika mpango huo vipo vijiji vinne ambavyo havikuwekwa kwenye mpango, sijui sababu ni nini. Vijiji hivyo ni Kelemakuu, Birise, Muungano na Sankaleti. Nataka kujua, Serikali ina mpango gani sasa wa kuviingiza vijiji hivyo kwenye mpango wa REA? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Monni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba vijiji hivyo vinne vya Kilemakuu pamoja na vingine vyote vipo katika hivyo vijiji 12 ambavyo vimebakia katika utekelezaji wa mradi na kufikia hiyo tarehe 31 Oktoba vitakuwa pia vimewashiwa umeme. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kasinge.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Usimikaji wa nguzo katika Kata ya Likawage na Vijiji vyake vya Nainoku, Liwiti na Likawage yenyewe katika Jimbo la Kilwa Kusini umekwama kutokana na changamoto ya *TFS* kuzuia kupitisha nguzo katika eneo la hifadhi. Je, ni nini mpango wa Serikali wa kushirikiana kati ya Wizara ya Nishati na Wizara ya Maliasili na Utalii kuondoa utata huu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kassinge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli, awali kulikuwa kuna changamoto kubwa ya Sheria ya *TFS* ambayo ilikuwa inatutaka sisi Wizara ya Nishati au watumiaji wengine wa maeneo yao kulipia gharama fulani lakini baada ya majadiliano tumekubaliana kwamba, kwa sababu tunafanya miradi ya Serikali kwa pamoja basi tupeane hizi *leeway* kwa ajili ya kupitisha hii miundombinu. Kwa hiyo, *case by case* zikitokea tunazi-*solve* kulingana na maeneo husika. Nitawasiliana na Mheshimiwa Mbunge ili tuone wapi tulipokwama na tuweze kutatua tatizo hili kwa sababu maeneo mengine tayari tumelimaliza.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hawa.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kumekuwa na changamoto kubwa ya kurukwarukwa kwa kuwekewa umeme kwa wananchi katika Kata za Kalunde na Ndevelwa katika Jimbo la Tabora Mjini. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwawekea wananchi wote umeme kwa usawa ili waweze kunufaika na huduma hii? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hawa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba hatujaweza kama Serikali kuwa na uwezo wa kumuunganishia kila mwananchi anayehitaji umeme leo, lakini mpango mkubwa wa Serikali ni kutafuta shilingi takribani trilioni sita na bilioni kama mia tano ambazo zitafikisha umeme kila kitongoji katika nchi hii, kila mtaa katika nchi hii. Hivyo, tunaamini wananchi walio wengi kwenye maeneo hayo wataweza kuupata umeme kwa wakati mmoja. Kwa sasa, kwenye mradi tuliokuwa nao wa *REA III round II,* tunaenda na wananchi wachache kama *sampling* kwa ajili ya kuhakikisha kwamba mradi umeanza, lakini tunaendelea kuongeza kuwafikia wananchi wengine kwa kadri ya uongezekaji wa bajeti.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Wananchi wa Kijiji cha Nyabikurungo Kata ya Ukuraijo waliwekewa nguzo na baadaye zikaondolewa bila kuunganishiwa umeme lakini pia Kijiji cha Bugaza, Kata ya Kimuli. Nataka kujua ni lini hawa wananchi watawashiwa umeme katika hayo maeneo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anatropia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba programu yetu ya kupeleka umeme vijijini itakamilika mwezi Disemba mwaka huu. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba kijiji hicho pia kitapata hiyo nishati ya umeme na mkandarasi anayepeleka umeme wa Rukomi na Kawahya tutamsimamia ili aweze kufanya kazi hiyo kwenye maeneo hayo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Kilimo. Mheshimiwa Asia.

Na. 31

**Ujenzi wa banio la maji Kata ya Endagau**

**MHE. ASIA A. HALAMGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Banio la Maji, Kata ya Endagau, Wilaya ya Hanang?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Asia Abdukarimu Halamga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Ujenzi wa Skimu ya Umwagiliaji *Endagaw* iliyopo katika Mkoa wa Manyara, Wilaya ya Hanang ulianza mwaka wa fedha 2021/2022. Hadi sasa Serikali imeshakamilisha ujenzi wa baadhi ya maeneo ikiwemo ujenzi wa ukuta wa bwawa wenye takribani mita 270 pamoja na punguza maji (*Spillway*) na baadhi ya maumbo ya mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imepanga kukamilisha

ujenzi wa kazi zote zilizobaki, hii ni baada ya kukamilisha mapitio ya usanifu wa mradi huu, ikiwemo mfereji wa Onjae pamoja na maumbo yake.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asia.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nichukue nafasi hii mimi pamoja na wananchi wa Kata ya Endagaw na wananchi wa Wilaya ya Hanang, kuiomba Serikali kuhakikisha kwamba ujenzi huo wa mifereji unafanyika sasa na sio kipindi cha masika kwa sababu sisi tunajua uhalisia wa jiografia tunapotoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; kwa kuwa wananchi wa Wilaya ya Hanang ni wananchi ambao wanalima sana. Je, Serikali haioni haja sasa ya kuendelea kuongeza mabwawa ili wananchi wa Wilaya ya Hanang waweze kulima kilimo cha uhakika na chenye tija? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, baada ya kumwondoa mkandarasi aliyeshindwa kufanya kazi yake vizuri, hivi sasa tunahakikisha kwamba mkandarasi ambaye tutamtangaza aifanye kazi hii kwa haraka na kuwahi msimu huo ambao umekuwa na athari kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Waziri, la pili, ni kweli Wilaya ya Hanang ina wakulima wengi. Katika mpango wa Serikali, mwaka huu wa fedha tutakwenda kuchimba bwawa eneo la Laganga ambapo zaidi ya hekta 600 za umwagiliaji zitapatikana na wakulima wa eneo la Hanang watapata maeneo ya kilimo chao cha umwagiliaji. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ndaisaba. Jiandae Mheshimiwa Yustina.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Serikali kupitia Wizara ya Kilimo mradi wake wa *DASP* walifika Ngara mwaka 2015, wakaanza kujenga Skimu ya Umwagiliaji ya Vigombo, wakaitelekeza ikiwa imefika katikati kwa zaidi ya miaka nane iliyopita. Je, ni lini Wizara ya Kilimo itafika Ngara na kuja kukamilisha Mradi wa Skimu ya Umwagiliaji ya Vigombo? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhamira ya Serikali kuhakikisha miradi yote ya umwagiliaji inakamilika na ndiyo maana tumewekeza fedha nyingi kwa ajili ya ukarabati na kuipitia. Nichukue fursa hii kumuahidi Mheshimiwa Mbunge ya kwamba nitampa maelekezo Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji aelekee katika eneo la Rulenge pale Vigombo ili aangalie mradi huu na tuone namna ya kuweza kuwakwamua wananchi ili wafanye kilimo cha umwagiliaji.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rahhi.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya swali la nyongeza. Je, ni lini Serikali itakamilisha kujenga miundombinu ya umwagiliaji, hasa kusakafia mifereji mikuu katika Skimu ya Mangisa na Diri iliyoko Wilayani Mbulu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, tumeendelea kuipitia miradi yote ya skimu za umwagiliaji ambayo ilikuwa ina changamoto na tumetenga fedha za mwaka huu na mwaka wa fedha ujao. Hivyo, nitakaa na Mheshimiwa Mbunge kuangalia katika mwaka huu kama haijawekwa kwenye bajeti hii, basi tuitengee bajeti inayokuja ilimradi tu wakulima waweze kupata fursa ya kufanya kilimo cha umwagiliaji.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Ndulane.

Na. 32

**Serikali kutatua kilimo cha pamba katika Wilaya ya Kilwa**

**MHE. FRANCIS K. NDULANE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itafufua kilimo cha pamba katika Wilaya ya Kilwa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, Mbunge wa Kilwa Kaskazini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kilwa ni miongoni mwa maeneo yaliyo chini ya karantini ya pamba katika eneo la kusini mwa Tanzania kutokana na uwepo au kupakana na nchi zilizoathiriwa na funza mwekundu *(diparopsis castenea)* ambaye ni mdudu hatari wa zao la pamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2020/2021 Serikali ilifanya tathmini ya hali ya funza mwekundu na kubaini kuwa mdudu huyo bado yupo katika maeneo ya karantini. Aidha, Wizara itaendelea kufanya utafiti kwa kushirikiana na Taasisi za Kimataifa kuhusu namna bora ya kudhibiti mdudu huyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ndulane.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naona majibu ya Mheshimiwa Waziri yamekuwa mepesi sana. Hii changamoto ya funza mwekundu iligundulika kwenye miaka ya 1940, sasa ni miaka zaidi ya 80 imepita bado hatujapata *solution* kuhusiana na changamoto hii. Je, Serikali ina mikakati gani

madhubuti, ningeomba tuelezwe kwa kutumia teknolojia ya kisasa kuweza kutatua changamoto hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; ningependa kujua, kuna mazao mengina ya michungwa, ufuta na minazi ambayo yanalimwa sana katika Wilaya ya Kilwa, ningependa kutaka kujua, je, Serikali imeishirikisha vipi taasisi *TARI* katika kutatua matatizo ya magonjwa ya mazao haya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli mdudu huyu alitambulika muda mrefu na kama Serikali tumeendelea kuwekeza katika kufanya utafiti kushirikiana na wadau wengi wa kimataifa. Lengo letu ni kuhakikisha kwamba tunamtokomeza mdudu huyu ambaye kila muda anaendelea kujipa maumbo tofauti tofauti lakini wataalam wetu wa *TARI* pamoja na wataalam wengine tunaendelea kuifanya kazi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo kubwa ni kuhakikisha tunamtokomeza mdudu huyu ambaye ana athari kubwa katika uzalishaji wa zao la pamba. Hivyo, nimwombe Mheshimiwa Mbunge, kwa sababu hivi sasa Mheshimiwa Rais ametoa fedha nyingi kwenye utafiti, tunaamini kupitia fedha hizi wenzetu wa *TARI* pamoja na mashirika mengine tutafanya kazi hii kwa uaminifu mkubwa kabisa ili mwisho wa siku tupate suluhisho la mdudu huyu na wakulima hao kama ambavyo dhamira yao ya kulima basi tuwe tumemtokomeza mdudu huyu.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili, bajeti yetu ya eneo ya utafiti miaka miwili iliyopita ilikuwa ni shilingi bilioni 11.6. Hivi sasa bajeti yetu ni shilingi bilioni 43 kwenye utafiti. Moja ya maeneo makubwa ambayo tumeyapa kipaumbele ni kuhakikisha pia tunakuja na namna bora ya udhibiti wa magonjwa na wadudu wasumbufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimhakikishie Mbunge kwamba, *TARI* imewezeshwa na hivi sasa inaendelea kufanya tafiti ili kuja na suluhisho la kudumu la magonjwa ambayo yamekuwa yakitatiza sana michungwa na minazi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Tendega.

Na. 33

**Upatikanaji wa *data* za bidhaa za kilimo zinazosafirishwa nje**

**MHE. GRACE V. TENDEGA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha inapata *data* za bidhaa zote za kilimo zinazosafirishwa nje ya nchi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Grace Victor Tendega, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inaendelea kuboresha mfumo wa *Agricultural Trade Management Information System (ATMIS)* kwa ajili ya kuufungamanisha na mfumo wa pamoja wa forodha wa Tanzania *(Tanzania Custom Intergrated Systems - TANCIS)* wa Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)*. Kufunganishwa kwa mfumo wa *ATMIS* na *TANCIS* kutaboresha upatikanaji wa takwimu za mazao na bidhaa za kilimo zinazoingizwa au zinazosafirishwa nje ya nchi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tendega.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili

ya nyongeza. Tumekuwa tukiona wanunuzi kutoka nje ya nchi wakija kununua mazao moja kwa moja wakiwa na magari yao ambayo yana namba za nje ya nchi; na tumekuwa tukiona wananchi wanauziwa kwa bei za chini sana, hasa mazao ya parachichi na mazao mengine kwa sababu hawana mtu anayewasimamia vizuri. Je, mnunuzi anapoenda kununua mazao hayo moja kwa moja kwa sasa hizo *data* wanazichukuwaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa Serikali imekiri kabisa inaendelea kuboresha huo mfumo wa *ATMIS* na *TANCIS* ni lini maboresho hayo yatakwenda kukamilika kwa sababu tumeona kwamba, bidhaa zinaenda nje ya nchi na tumekuwa hatujui mchango kamili wa kilimo kwa fedha za kigeni.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la kwanza, ni kweli kumekuwepo na baadhi ya wanunuzi ambao wanakwenda moja kwa moja mashambani, ndiyo maana Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka tulileta utaratibu wa namna ya ununuzi wa mazao ili wale wote ambao wanataka kununua mazao nchini Tanzania wafuate utaratibu na mwisho wa siku sisi kama Serikali tupate takwimu sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa Serikali ni nini katika hili. Jambo la kwanza, katika eneo la mazao ya nafaka, hivi sasa tunataka kuboresha, kutengeneza masoko ili bidhaa zote zipelekwe katika masoko na wanunuzi wakanunue katika masoko yanayotambuliwa ili kupata takwimu sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, kwenye mazao ya mbogamboga na matunda, hivi sasa tunajenga *common use facilities* tatu za kuanzia katika eneo la Nyororo, Hai na Kurasini, ambapo kwa mfano parachichi yote itakusanywa, tutafanya *grading, sorting* na *packaging* ambayo itatupa pia uhakika wa kujua ni parachichi kiasi gani imekusanywa na kupelekwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, swali lako la pili kuhusu mifumo hii, kama mnavyofahamu Waheshimiwa Wabunge mifumo hii siyo jambo la siku moja. Tunaendelea kuiboresha kutokana na maendeleo ya teknolojia vilevile na ukuaji wa soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano kwa hivi sasa, tunao mfumo wetu ukiacha hii mifumo mingine wa kutumia mamlaka ya afya, mimea na viuatilifu, ambao wao wanawajibu wa kutoa *phytosanitary* kwa bidhaa zozote ambazo zinatoka nje ya nchi, cheti cha usafi wa mazao pia na wenyewe ni mfumo ambao tumewaunganisha kutupa takwimu sahihi. Kwa hiyo, hakuna mtu aliye na uwezo wa kusafirisha mazao nje ya nchi kama hajapata *export permit* na *phytosanitary certificate* ambayo pia inatupa nafasi ya kuweza kujua ni mazao kiasi gani yamesafirishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutaendelea kuboresha mfumo huu ili tupate takwimu sahihi ya mazao yetu.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa jibu zuri, ameshakuelewa. Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Michezo. Mheshimiwa Gwajima.

Na. 34

**Matumizi ya bahari kwa michezo**

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itakuja na mpango wa kuitumia Bahari kwa michezo mbalimbali ya majini ili kuongeza kipato cha wananchi wa Jimbo la Kawe?

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa

Askofu Josephat Mathias Gwajima, Mbunge wa Kawe, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sera ya Maendeleo ya Michezo ya Taifa ya mwaka 1995, Ibara ya 7(i) hadi (vi), jukumu la ujenzi na uendelezaji wa miundombinu ya michezo ni jukumu la Serikali Kuu, Mamlaka ya Serikali za Mitaa pamoja na wadau wa sekta ya michezo zikiwemo taasisi, mashirika na watu binafsi. Hata hivyo, Wizara kupitia Baraza la Michezo la Taifa (BMT) na kwa kushirikiana na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania *(TFF)* wako katika mkakati wa kuziendeleza fukwe za Kunduchi na Kigamboni katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo ni kukuza mchezo wa Soka la Ufukweni ambao tayari *TFF* wameshaanzisha Ligi yake ambayo ilianza tangu Tarehe 19/08/2023 na inafanyika kwa siku za Jumamosi na Jumapili katika fukwe za Koko, na jumla ya Timu 16 zinashiriki Ligi hiyo. Aidha, naomba niliarifu Bunge lako Tukufu kuwa mwezi Julai, 2023, Timu ya Taifa ya Soka la Ufukweni ilishiriki mashindano ya mchezo huo Barani Afrika yaliyofanyika Nchini Tunisia na kushika nafasi ya tatu, nyuma ya Morocco na Senegal.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatoa rai kwa wadau wa michezo mingine kama Mitumbwi na Ngalawa, Kuogelea, Mpira wa Kikapu na Wavu kuwekeza katika michezo hii ya ufukweni na kuziendeleza fukwe tulizonazo ili kukidhi matakwa ya michezo yao, kwani pamoja na kuongeza kipato kwa wananchi, michezo hii pia inasaidia kuimarisha afya na kutoa burudani kwa wananchi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gwajima.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; kwa kuwa nusu ya Jimbo la Kawe kwa maana ya Msasani, Masaki, *Oysterbay*,

Kunduchi, Mbweni, Kawe, Bunju, *Sea Cliff* na Coco yote iko katika ufukwe wa Bahari ya Hindi. Je, Serikali ina mpango gani maalum wa kuendeleza hii michezo ya Bahari kwa ajili ya afya, burudani na kipato cha watu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Mheshimiwa Naibu Waziri, je, utakubali Jumapili hii tuandamane pamoja tukafungue Ligi ya Rede kwa michezo inofanyika katika Jimbo la Kawe? *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba kuchukua nafasi hii ya kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, Josephat Gwajima kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpe pongezi Mheshimiwa Mbunge kwa kuwa miongoni mwa viongozi wa kwanza kwa kuona fursa kubwa iliyopo katika mchezo wa soka la ufukweni.

Mheshimiwa Naibu Spika, soka la ufukweni katika nchi hii limeanzishwa rasmi mwaka 2014 na ni kwa miaka tisa tu ambayo tumekuwa tukilifanya, lakini limeonyesha kuwa na mafanikio makubwa. Kwa sasa tuko Namba Tano kwa Bara la Afrika kwa soka la ufukweni na Namba 42 kwenye *rank* za *FIFA* za kidunia kwa soka la ufukweni, namba ambazo hili soka letu la kawaida hatujawahi kuzifikia na pengine itatuchukua muda mrefu kidogo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia mafanikio haya yanatokana na uwekezaji mkubwa unaofanywa na *TFF* kwa kushirikiana na Serikali, kutekeleza maelekezo ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kuhakikisha tunaweka mkazo kwenye michezo yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *TFF* wanao mpango mkakati wa miaka mitano, ambao pamoja na mambo mengine unahakikisha

kwamba soka la ufukweni linafundishwa mashuleni na vyuoni na kila Mkoa ambao una fukwe kuweza kuwa na ligi yake kwa ajili ya soka la ufukweni. Lengo ni katika kipindi cha miaka mitano hii inayofuata tuwe na wachezaji angalau 10,000 na kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Serikali imeanzisha mazungumzo na JKT na wadau wengine kadhaa ili kuhakikisha tunaongeza uwekezaji kwa ajili ya soka la ufukweni. Pia, kumekuwa na mashindano ya *Copa Dar es Salaam* ambayo yanazishirikisha nchi mbalimbali kama Burundi, Uganda, Comoro, Ushelisheli na Malawi, mwaka huu tuna mpango wa kuwaalika Kenya, Oman, Morocco na Senegal. Kwa hiyo, tutakuwa na Ligi ya Soka la Ufukweni yenye nchi Tisa, ambapo ni wazi kabisa itaongeza Pato la Taifa lakini wachezaji wetu wengi watashiriki na itatoa ajira za moja kwa moja na ajira nyingi nyingine zinazozunguka mchezo huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali lake la pili, najua Askofu utakuwa na maono, umengundua kama Jumapili ninao muda na tutaambatana mimi na wewe kwa ajili ya kwenda kuanzisha Ligi yako ya rede pale Jimboni Kawe. Ahsante. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea Wizara ya Maliasili na Utalii.

Na. 35

**Kuzuia wafugaji kuchungia katika Hifadhi ya Julius Nyerere**

**MHE. ALEKSIA A. KAMGUNA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuzuia wafugaji kuchunga mifugo katika Hifadhi ya Julius Nyerere?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aleksia Asia Kamguna, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Uhifadhi Wanyamapori Sura Namba 283 iliyorejewa mwaka 2022, Sheria ya Hifadhi za Taifa Sura 282 na Sheria ya Misitu ya mwaka 2002, zimeweka zuio la kuingiza mifugo ndani ya maeneo ya hifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya uingizaji wa mifugo katika maeneo yaliyohifadhiwa ikiwemo Hifadhi ya Taifa Nyerere ni ya muda mrefu. Wizara inakabiliana na changamoto hii kwa kuimarisha doria katika maeneo ya hifadhi na kuwachukulia hatua wanaoingiza mifugo hifadhini kwa mujibu wa Sheria na Kanuni zilizopo. Aidha, Wizara inaendelea kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kukabiliana na changamoto hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aleksia.

**MHE. ALEKSIA A. KAMGUNA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kwenye mbuga zetu kuna Askari pamoja na Maafisa wengine ambao wanazilinda hizo mbuga. Ukienda kule kwenye mbuga utakuta kuna vibanda vya wafugaji wanaishi huko pamoja na rundo la mifugo wakati Serikali wanasema kwamba wameweka zuio. Je, hao wafugaji walioko kule na hivyo vibanda hawa Askari hawawaoni? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili. Inasemekana kuna baadhi ya Maafisa Wanyamapori ambao siyo waaminifu, wanashirikiana na wale watu wenye mifungo kuwaingiza katika hifadhi zetu. Je, Serikali inasemaje katika hili? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Aleksia Kamguna, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba hawa Askari wanakuwepo katika maendeo ya hifadhi, changamoto ambayo tunakutana nayo hasa kwenye mapori ambayo yameungana na mapori ya Halmashauri na mengine ni mapori ya Vijiji. Kwa mfano, kama Hifadhi ya Nyerere, tuna Hifadhi ya Selous lakini kuna mapori ambayo yameungana na Hifadhi ya Nyerere. Kwa hiyo, utakuta kwamba kwenye Pori la Selous Askari wanafanya operesheni, pale ambapo kunakuwa na mifugo, inakamatwa na inachukuliwa hatua lakini wale wamiliki wahiyo mifugo wanaenda wana-*pause* kwenye yale mapori ya Halmashauri pamoja na Vijiji ambapo sasa kule askari wetu hawafiki katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, changamoto hiyo imekuwa kubwa kwa sababu hii mifungo ipo na inakuwa kando kando tu inakuwa imeegeshwa pale ambapo Askari wetu wanapoondoka tu tayari mifugo inaendelea kuingia hifadhini, lakini kulingana na sheria zetu, nadhani wanafahamu wafugaji namna ambavyo tunasimamia kanuni, taratibu na namna ambavyo tunaendelea kuzishughulikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hili suala la Askari kushirikiana na Wafugaji. Ni kweli tuna sheria kali sana na pale inapogundulika kwamba Askari anashirikiana na kukiuka kanuni na taratibu zilizopo, tunamchukulia hatua mara moja na wengine wanafukuzwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii sheria tunatumia Sheria ya Jeshi ambayo tayari sisi tumeshaanza kuingia katika utaratibu huu na wengi wameshachukuliwa hatua. Kwa hiyo, ikithibitika kwamba kuna Askari amefanya hivi basi tupate taarifa mara moja na tuweze kuchukua hatua. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Riziki Lulida.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Lindi sasa hivi, eneo la Selous pamoja na Mbuga ya Tendeguru kuvamiwa na wafugaji. Mheshimiwa Naibu Waziri ni shahidi, alikwenda akawakuta wafugaji wako ndani ya mbuga, wakichoma mikaa katika Misitu ya Tendeguru na kumaliza Miti ya Mipingo lakini kusababisha sasa hivi taharuki, Wafugaji kutoka katika misitu, kwenda kuvamia mashamba ya watu. Sasa hivi Mkoa wa Lindi tuko katika taharuki kubwa ya mapigano ya wafugaji na wananchi.

Je, Mheshimiwa Waziri aliyepo pale anatoa tamko gani leo hapa kwa vile aliyaona haya lakini utekelezaji wake haukukamilika mpaka hivi sasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha swali langu. Ahsante.*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Sisi kama Serikali tumeshajipanga, kwa maana ya Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, tukae pamoja kwa sababu suala hili ni suala la wananchi wetu na hao wananchi nao wanayo haki ya kuishi kama Watanzania. Tunachokifanya sasa hivi tunasimamia sheria upande mmoja lakini upande wa pili wanaegesha tu wanasubiria kuingia tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo sisi kama Serikali tukae pamoja, tuone namna iliyo bora ya kuwahudumia hawa wafugaji ili changamoto hii sasa isiendelee kujitokeza. Kwa sababu sasa hivi sisi tumepewa dhamana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri, umejibu vizuri, kaeni pamoja sasa. Mheshimiwa Catherine Magige.

Na. 36

**Kudhibiti wanyama wanaoharibu mazao Kata za Monduli**

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE** aliuliza: -

Je, upi mpango wa kudhibiti wanyama wanaoharibu mazao na kugharimu maisha ya watu Kata za Naarami, Lokisale, Moita, Lepruko na Makuyuni?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Catherine Valentine Magige, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, mwingiliano kati ya binadamu na wanyamapori umekuwepo kwa muda mrefu. Hata hivyo, miaka ya hivi karibuni mwingiliano huo umeongezeka na kusababisha madhara kwa wananchi ikiwa ni pamoja na kuua mifugo na kuharibu mali za wananchi ikiwemo mazao na wakati mwingine kusababisha vifo au kujeruhi wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia kuwepo kwa changamoto ya wanyamapori wakali na waharibifu, Wizara imeandaa mpango wa kongoa shoroba katika maeneo mbalimbali nchini, ikiwemo Kata za Naarami, Lokisale, Moita, Lepruko na Makuyuni. Aidha, Wizara imewaelekeza wananchi kuacha kuanzisha shughuli za kibinadamu kwenye mapito ya wanyamapori ili kuepuka madhara yanayotokana na wanyamapori hao.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Magige.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Naibu Spikja, ahsante, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni nimefanya ziara Wilayani Monduli na moja kwa moja Mheshimiwa Waziri wa Maliasili alizungumza na wananchi wa Monduli, akawaahidi baada ya wiki moja ya ziara yangu ataenda na wataalam wake kutatua kero hii, lakini mpaka leo hii Waziri hajaonekana. Matokeo yake mwezi uliopita mwananchi mmoja katika Kata ya Makuyuni eneo la Ndoroboni ameuawa na tembo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tatizo la tembo limekuwa kero kubwa sana kwa Tanzania nzima, wamekuwa wanazagaa zagaa ovyo na kuharibu mazao na kuua wananchi, Serikali imekuwa inatupa majibu hatuoni matokeo yake. Sasa leo nataka kufahamu nini kauli ya Serikali? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ni kweli kumekuwa na tatizo hili la changamoto la wanyama wakali na waharibifu, ni changamoto sasa takribani miaka minne inaendelea kuongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imechukua hatua za haraka. Moja ya hatua za haraka ni kwamba tumeanza sasa hivi kuwarudisha hawa wanyama wakali kwa kutumia helikopta, kuna baadhi ya maeneo tayari tulishaanza kwenda. Wakati huo huo tunaendelea kutoa elimu kwa wananchi kwa sababu ukiangalia maafa kwa asilimia kubwa yanajitokeza ni pale wananchi hawana elimu, wengine wanafukuza kwa kutumia fimbo na kadhalika. Kwa hiyo tunaendelea kuitatua hii changamoto wakati huo huo na kutoa elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua nyingine ya haraka ni kwamba sasa hivi tumeamua tutapeleka Askari ambao watakaa

katika maeneo husika kwa muda mrefu. Suala la kupigia simu Askari ndiyo wafike sasa hivi tunataka kuliacha na tunataka hawa Askari kwenye maeneo yale hatarishi wakae maeneo yale wakishirikiana na wale *VGS (Village Scouts)* ili kuondoa hili tatizo kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tuna operesheni ambayo tumeipanga na Mheshimiwa Waziri ameelekeza na tayari tutaingia kazini mara moja. Kwa hiyo, naomba niwatoe wasiwasi wananchi kwamba Serikali inalishughulikia suala hili kwa karibu sana na haya ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais, pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu, umetuelekeza tulishughulikie kwa uharaka, tunatambua wananchi wanaumia lakini naomba nitoe kauli hii kwamba wananchi tutawafikia muda siyo mrefu. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ahsante. Waheshimiwa Wabunge najua kero hii ipo maeneo mengi na hivi karibuni wameonekana Dodoma na Serikali iko kazini inafanya kazi kuhakikisha inadhibiti, jibu hili ndiyo liwe jibu sahihi la Serikali. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea Wizara ya Maendeleo ya Jamii na Jinsia, Mheshimiwa Gwau.

Na. 37

**Makazi ya kuwahifadhi waliofanyiwa ukatili**

**MHE. MARTHA N. GWAU** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga nyumba za kuwahifadhi waliofanyiwa ukatili ikizingatiwa kuwa ukatili kwa watoto na wanawake umeongezeka?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Martha Nehemia Gwau, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mpango wa kuwahifadhi waliofanyiwa ukatili (kujenga nyumba za kuwahifadhi waliofanyiwa ukatili), Serikali imeandaa Mwongozo wa Uanzishaji na Uendeshaji wa Nyumba Salama wa Mwaka 2019, kwa ajili ya manusura wa vitendo vya ukatili pamoja na wahanga wa biashara haramu wa usafirishaji wa binadamu. Lengo ni kuweka mazingira wezeshi kwa uanzishaji huduma ya nyumba salama kwa manusura wa ukatili wa kijinsia na kwa watoto hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hadi kufikia June 2023 jumla ya nyumba salama 12 zimeanzishwa na kusajiliwa katika Mikoa ya Arusha, Kigoma, Kilimanjaro, Dar es Salaam na Mwanza. Serikali itaendelea kushirikiana na wadau wa sekta binafsi kuhakikisha upatikanaji endelevu wa huduma hii kwa mujibu wa Mwongozo wa mwaka 2019.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Martha Gwau.

**MHE. MARTHA N. GWAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa katika mikoa 12 iliyotajwa ya hizo nyumba, Mkoa wa Singida siyo miongoni mwa Mikoa iliyo na hiyo huduma. Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha nyumba hizo katika Mkoa wa Singida?

Swali la pili, kwa kuwa ukatili kwa watoto bado unaendelea siku hadi siku. Je, Serikali imefikia wapi au ina mpango gani wa kuanzisha Vituo vya Kulelea Watoto *(ECD Centers)* ili kuhakikisha kwamba wazazi wanakuwa wanawaacha watoto kwenye mikono salama? Nashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana,

naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Nehemia Gwau:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kujenga nyumba salama katika Mkoa wa Singida, ni dhahiri kwamba iko mikoa mingi kweli ambayo haina nyumba salama, hapa ni mitano tu inayo, na wizara inafanya jitihada za kuwasiliana na wadau ambao wamekuja kutusaidia katika mapambano haya ya kutokomeza ukatili. Andiko hilo likipita, tutapeleleka hizi rasilimali katika maeneo ambayo yana uhitaji mkubwa ikiwemo huko Singida.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kupitia mwongozo huu, tunaomba mamlaka za Mikoa na Halmashauri na wadau walioko huko waone umuhimu wa kuanza kuanzisha nyumba hizi wakati Wizara inakuja kuongezea nguvu. Vilevile kwenye bajeti zinazokuja; mwaka ujao tutaendelea kutenga fedha kidogo katika ngazi zote kwa ajili ya kuchochea ujenzi wa nyumba Salama hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kuhusu maelezi ya Watoto, ni kweli, mpango wa Serikali ni kuhakikisha watoto wanalelewa vizuri kwa kuwajengea vituo vya kuwalea na kuwakuza katika maeneo ya jamii. Sasa tuna vituo 200 tumeshirikiana na wadau kuvijenga. *Formular* ni ile ile, tunahamasisha wadau waliopo kwenye Halmashauri zetu waendelee kujitokeza na kuchangia fedha kwa ajili ya vituo hivi, lakini kwenye bajeti zetu tutatenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia hivi sasa Wizarani tuna kikao kinaendelea cha *resource mobilization*. Hivyo, tukiipata, tutaanza kuwapelekea wale ambao wameshamiliki na wameanza huku tukiwaelimisha wengine ambao bado hawajaona umuhimu huo, kuamka na kujipanga kwenye bajeti za mwaka unaokuja, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Toufiq.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Baadhi ya wahanga wa ukatili wamekuwa wakirushwa picha zao katika mitandao hivyo

kutwezwa utu wao; na hivyo kusababisha baadhi ya ambao wanafanyiwa ukatili kutokutoa taarifa: Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusiana na jambo hili?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Toufiq kuhusu hao wanaopiga picha mitandaoni, kweli inasikitisha sana. Serikali imekuwa ikitoa maelekezo na maagizo ya kwamba waache kufanya hivyo, na wamekuwa wakiendelea. Sasa kauli ya Serikali ni kwamba, vitendo hivyo ni vibaya katika malezi, makuzi na maadili ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vitendo hivyo vinawaharibu watoto wetu ambao ni Taifa la kesho. Kwa sababu wamekuwa hawasikii, sasa hili ni onyo la mwisho, vinginevyo nakwenda kuita kikao cha wadau wote na wote hao waliopiga hizo picha za namna hiyo, nitaongoza kwenda kuwashitaki kwa mujibu wa sheria kwenye Jeshi la Polisi ili sheria zetu tulizozitunga wenyewe zifanye kazi yake, zisikae tu kabatini. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa. Tunaendelea na Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Mpakate.

Na. 38

**Ujenzi wa Mahakama Tarafa za Tunduru**

**MHE. DAIMU I. MPAKATE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Mahakama katika Makao Makuu ya Tarafa za Nalasi, Lukumbule na Namasakata – Tunduru?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, Mbunge wa Tunduru Kusini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahakama inaendelea na utekelezaji wa Mpango wa ujenzi wa Mahakama hizi ambapo Mahakama ya Mwanzo ya Nalasi inajengwa katika mwaka huu wa fedha 2023/2024 ikiwa ni sehemu ya Mahakama za Mwanzo 71 zitakazojengwa nchi nzima. Tayari Mshauri Mwelekezi ameanza kufanya kazi, na mradi unatarajiwa kuanza Oktoba, 2023 na kukamilika kabla ya Juni, 2024. Mahakama za Mwanzo za Lukumbule na Namasakata zitaingizwa kwenye mpango ujao wa miaka mitano sambamba na tarafa nyinginezo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika bajeti ya mwaka huu wa fedha moja ya Mahakama za Wilaya zitakazojengwa ni Wilaya ya Tunduru, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mpakate.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naishukuru Serikali kwa majibu mazuri sana, na tunaomba waendelee kumalizia hiyo Mahakama. Nina swali moja tu la nyongeza. Kwa kuwa maeneo ya Lukumbule na Masakata na Nalasi yamekosa kabisa huduma za kimahakama: Je, Serikali haioni sasa kuna haja ya kuweka *Mobile Court* katika tarafa hizi ili ziweze kupata huduma za kimahakama? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza tunashukuru kwa pongezi na shukrani hizo. Kwa sasa Mhimili wa Mahakama una magari mawili *(mobile courts)* ambazo zinafanya kazi Mkoa wa Dar es Salaam na

Mkoa wa Mwanza. Katika bajeti yetu tunategemea kuongeza hizi *mobile courts* sita Mikoa ya Kagera, Tanga, Dodoma, Arusha, Mara na Morogoro. Tunafanya hivi kwa maeneo ambapo *population* ni kubwa. Tunatamani tungefika kwa kila Kata, lakini mwenendo wetu wa huu mpango wa Mahakama ni kujenga Mahakama hizo kwa sababu hizi *mobile courts* ni gharama kuziendesha na wakati mwingine *management* ya mahabusu na mambo mengine yanaweza yakawa yanaleta gharama kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namuahidi tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Kata zake hizi ambazo amezitaja, tutaingiza katika mwaka ujao wa fedha, na tutafikia Kata zake na tutazijenga kwenye maeneo ambapo uhitaji upo, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Issaay, halafu jiandae Mheshimiwa Sophia.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Mahakama ya Wilaya ya Mbulu ni Mahakama chakavu sana iliyojengwa toka enzi za mkoloni; na ni miaka mitatu nimekuwa nikiendelea kuomba ujenzi wa Mahakama hiyo: Je, Serikali ina mpango gani wa kutujengea Mahakama Wilaya ya Mbulu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba nijibu swali la Mheshimiwa Issaay Mbunge wa Mbulu Mjini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka huu wa fedha, miongoni mwa maeneo tutayokwenda kujenga, tunategemea kujenga Mahakama 18 za Wilaya. Wilaya ya Mbulu ni miongoni mwa Wilaya ambazo tutajenga Mahakama hii. Kweli eneo lao lile, jengo la Mahakama lipo pembeni ya barabara na kimsingi linatakiwa litoke pale. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba

huu mpango tunao na tutajenga katika mwaka huu wa fedha. Upo kwenye *list* yetu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Chumi.

Na. 39

**Biashara ya China na Tanzania kufanyika kwa shilingi**

**MHE. COSATO D. CHUMI** aliuliza: -

Je, Serikali ipo tayari kuandaa mazingira kuwezesha biashara kati ya China na Tanzania kufanyika kwa shilingi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cosato David Chusmi, Mbunge wa Mafinga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika biashara za Kimataifa, wafanyabiashara wanao uhuru wa kutumia sarafu yoyote inayorahisisha biashara na inayokubalika na nchi nyingine kwa lengo la kupunguza gharama za miamala na muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itafanyia kazi jambo hili ili kuona ni nini kinapaswa kufanyika kuwezesha wafanyabiashara wa nchi ya China kukubali matumizi ya sarafu ya Tanzania, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Sina swali la nyongeza isipokuwa ushauri kwa Serikali. Hilo jambo basi waweze kulifanyia

kazi kwa haraka kama litakuwa na lina matunda mema kama ambavyo watakuwa wamejiridhisha kulingana na Sera za Uendeshaji wa Serikali.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Viwanda na Biashara. Mheshimiwa Asenga.

Na. 40

**Kufufua Kiwanda cha *General Tyre* na Shamba la Mpira Kilombero**

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kufufua Kiwanda cha *General Tyre* na shamba la mpira Kata ya Mwaya-Kilombero?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, Mbunge wa Kilombero, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Kiwanda cha Matairi Arusha, uko kwenye hatua ya kukamilisha taratibu za kuutangaza ifikapo mwezi Oktoba, 2023 ili kuweza kumpata mwekezaji mahiri mwenye mtaji na teknolojia ya kisasa inayohitajika. Mradi huu unatarajiwa kutangazwa ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa mashamba ya mpira likiwemo shamba la Kilombero, Serikali kupitia Shirika la Taifa la Maendeleo *(NDC)* imeendelea kuboresha uzalishaji wa mpira kwa kupanda miche mipya, kujenga miundombinu, kununua mashine za kugemea utomvu, uchakataji na vitendea kazi vingine ili kuongeza upatikanaji wa utomvu na mpira mkavu wenye viwango bora, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asenga.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kufanya ziara jimboni karibu mara mbili, ametembelea kiwanda cha *Kilombero Sugar* na *Mang'ula Machine Tools* pamoja na shamba hili la *rubber*.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza. Shamba hili ambalo lina ukubwa wa karibu hekari 1,678; sasa hivi kuna watu wachache kwa manufaa yao wanalikodisha kwa wananchi: Kwanini Serikali kupitia Serikali ya Kata isitoe uwazi eneo la shamba ambalo halijapandwa *rubber,* lilimwe na wananchi mpunga au miwa kwa uwazi tofauti na ilivyo sasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Ili kuweka ulinzi wa shamba hilo, tuliwasilisha ombi letu kwa Mheshimiwa Waziri kutoa sehemu ya shamba kwa maslahi ya maendeleo ya wananchi kwa ujenzi wa kituo cha polisi, *high school* na kituo cha afya: Je, ombi letu limefikia wapi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ni kweli kulikuwa na changamoto hizi za uvamizi katika shamba hili la mpira. Namshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa kuleta taarifa hii ambayo kimsingi hairuhusiwi watu kufanya shughuli nyingine nje ya shughuli tarajiwa katika shamba hili la mpira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kuna uvamizi huo, naomba niielekeze *NDC* waweze kufuatilia ili kama kweli kuna haja ya wananchi kutumia maeneo ambayo hayajaanza kuendelezwa kwa kupanda miti ya mpira, basi tuone namna ya utaratibu mzuri kama ambavyo ameshauri Mheshimiwa Mbunge kupitia viongozi wa Kata

na eneo husika ili wananchi wa pale waweze kufaidika na kutumia eneo hilo ambalo ni la Serikali, kwa utaratibu kamili. Kimsingi, eneo hili ni la kuzalisha miti kwa ajili ya mpira.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili kama alivyosema Mbunge, Mheshimiwa Waziri amepitia katika shamba hili, tunaendelea kujadiliana tuone namna gani tunaweza kuwezesha huduma hizi za kijamii kwa maana ya shule, vituo vya afya au kituo cha polisi, tuone kama vinaweza kujengwa katika eneo hili la shamba ambapo kimsingi ni kwa ajili ya uzalishaji wa mpira, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mageni.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Je, ni nini mpango wa Serikali katika kufufua viwanda vilivyotelekezwa kwa muda mrefu kikiwemo kiwanda cha kuchambua pamba cha Nyambiti kinachopatikana katika Kijiji cha Mwabilanda katika Jimbo la Sumve?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Ni kweli moja ya maeneo ambayo Serikali tunaweka mkazo sasa ni kuona tunafufua viwanda ambavyo vilikuwa vimebinafsishwa, na baadhi ya maeneo au viwanda hivyo wale wawekezaji tuliowabinafsia hawajavifufua au kuviendeleza au wanafanya tofauti na mkataba tuliowapa. Pamoja na viwanda vingine, hiki pia kipo kwenye mpango huo ambapo tunaendelea kutafuta wawekezaji au kuhakikisha wale ambao tumewakabidhi kwa sasa, waweze kuviendeleza kulingana na mikataba ambayo tulikuwa tumeingia nao, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda wetu ndiyo umekatika. Nina matangazo. Tunaanza na tangazo la Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa mamlaka aliyokuwa nayo, amemkaimisha nafasi ya Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni, Mheshimiwa Kepteni Mkuchika. *(Makofi)*

Wageni walioko Bungeni; wageni 14 wa Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa Mbunge, Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi ambao ni Wakurugenzi, Wakuu wa Idara na Vitengo vya Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu, Ndugu Gabriel Migire (nimeambiwa yupo chumba hiki cha huku); Dkt. Ally Possi, Naibu Katibu Mkuu; Profesa Longinus Lutasitara, Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania *(TCAA);* na Ndugu Hamza Johari, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania *(TCAA)*. *(Makofi)*

Wengine ni wageni wawili wa Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, kutoka *Top Education Consulting Ltd.* Dar es Salaam, karibuni. *(Makofi)*

Wengine ni wageni 76 wa Mheshimiwa Kasalali Mageni, ambao ni watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba ,Mkoani Mwanza wakiongozwa na Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo. *(Makofi)*

Wapo wageni 15 wa Mheshimiwa Miraji Mtaturu, Wajumbe wa Taasisi ya Kumbukumbu ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Mkoa wa Singida. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Justin Nyamoga ambao ni wapiga kura wake kutoka Kilolo Mkoa wa Iringa. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Priscus Tarimo kutoka Jijini Dar es Salaam; na wageni watatu wa Mheshimiwa Michael Mwakomo ambao ni wapiga kura wake kutoka Kibaha, Mkoa wa Pwani, karibuni. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Minza Mjika ambao ni watoto wake kutoka Meatu Mkoa wa Simiyu. *(Makofi)*

Pia wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Charles Kajege ambao ni Wachungaji kutoka Mkoa wa Geita. *(Makofi)*

Yupo pia mgeni wa Mheshimiwa Mariam Nyoka ambaye ni Mtakwimu kutoka Temeke Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Katibu wa Bunge anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa tarehe 2 Septemba, 2023 kutakuwa na Bonanza la mwezi Septemba. Bonanza hili litafanyika katika viwanja vya Shule ya Sekondari John Merlin iliyoko Miyuji Jijini Dodoma. Bonanza litahusisha michezo mbalimbali ya burudani na mashindano na litaanza kwa maandamano yatakayoanzia Chuo cha Mipango Dodoma saa 12.00 asubuhi.

Waheshimiwa Wabunge wote mnakumbushwa kufanya maandalizi ya Bonanza hili kwa kufanya mazoezi bila kusahau kujisajili kwa mchezo unaopenda kushiriki.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* - KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Azimio la Bunge Kuhusu Mapendekezo ya Kuridhia Katiba ya Tume ya Usafiri wa Anga ya Afrika ya Mwaka 2009 *(The Constitution of the African Civil Aviation Commision, 2009)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri Ujenzi na Uchukuzi.

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha Azimio la kuridhia Katiba ya Tume ya Usafiri wa Anga ya Afrika ya mwaka 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kutumia fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema

kwa kutuwezesha kukutana tena kwenye Bunge lako Tukufu tukiwa na afya njema.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi na Mheshimiwa Spika kwa jinsi mnavyoendelea kulisimamia Bunge letu Tukufu. Aidha, ninawashukuru Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwa kusimamia kwa ufanisi mkubwa majadiliano yote yaliyofanyika kuhusu Mapendekezo ya Kuridhia Katiba ya Usafiri wa Anga ya Afrika ya Mwaka 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee nichukue fursa hii kumshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuongoza nchi kwa umahiri mkubwa. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi wanavyotekeleza majukumu yao kwa weledi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Umoja wa Afrika ulianzishwa tarehe 26 Mei, 2011 Jijini Addis Ababa, Ethiopia ambao unajumuisha mataifa huru 52 ya Afrika. *AU* ilitokana na Umoja wa Nchi Huru za Afrika ambao ulianzishwa tarehe 25 Mei, 1966.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, *AU* na iliyokuwa *OAU* imekuwa ikianzisha idara mbalimbali chini ya Umoja huo, ikiwemo Idara ya Nishati na Miundombinu. Chini ya idara hiyo, zilianzishwa taasisi mbalimbali ikiwemo Tume ya Usafiri wa Anga ya Afrika ambayo ilianzishwa tarehe 17 Januari, 1969. Lengo la taasisi hii ni kusimamia masuala ya Usafiri wa Anga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi hii ilianza kutekeleza majukumu yake kupitia Katiba ya mwaka 1969. Madhumuni ya *AFCAC* chini ya Katiba hiyo yalikuwa pamoja na yafuatayo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kuandaa mipango kwa ajili ya utoaji huduma kwa ajili ya Usafiri wa Anga ndani na nje ya Bara la Afrika; pili, kufanya utafiti kuhusu Usafiri wa Anga Barani Afrika; na kadhalika. Tanzania ili-*sign* Katiba hiyo tarehe 17 Januari, 1969.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza majukumu yake, Tume hiyo imepata mafanikio mbalimbali ikiwa ni pamoja na yafuatayo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kuziunganisha nchi wanachama katika kutetea maslahi ya Bara la Afrika katika nyanja ya usafiri wa anga; kuwezesha mamlaka za usafiri wa anga za nchi za nchi za wanachama kujadili na kupanga kwa pamoja shughuli za usafiri wa anga na kuratibu matumizi bora na uendelezaji ya mifumo ya usafiri wa anga katika nchi wanachama.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanachama wa Tume hiyo, chini ya Katiba ya mwaka 1969 ulisaidia kuleta mafanikio mbalimbali nchini Tanzania ikiwemo na yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kupata uwakilishi katika Baraza la Utendaji la *ICAO* kwa vipindi vinane tofauti ikiwemo vipindi viwili mfululizo kuanzia mwaka 2013 hadi 2016 na mwaka 2016 hadi 2019; Ofisi ya CAG kuteuliwa kuwa Mkaguzi wa Hesabu za Tume hiyo kwa kipindi cha mwaka 2018 hadi 2021 na kipindi cha 2022 hadi 2024. Mafanikio mengine ni kupata fursa za mafunzo kwa wataalamu 135 wa usafiri wa anga kwa kipindi mwa mwaka 2021/2022 na hivyo kuwawezesha Watanzania kuendelea kupata uzoefu katika nyanja za kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio mbalimbali yaliyopatikana na Tume hiyo chini ya Katiba ya mwaka 1969, taasisi hiyo ilikumbwa na changamoto mbalimbali zilizosababisha kupendekezwa kutungwa kwa Katiba ya mwaka 2009. Changamoto hizo ni pamoja na zifuatazo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kukoseka kwa Taasisi ya kusimamia utekelezaji kuhusu ulegezaji wa masharti ya usafiri wa anga barani Afrika; pili, kutokuwepo kwa Sheria na Kanuni zinazosimamia ushindani wa biashara ya usafiri wa anga zinazotoa fursa na usawa kwa wadau pamoja na kukuza ushindani; tatu, ushirikiano usioridhisha katika masuala ya kisekta kati ya nchi wanachama na Taasisi nyingine za kimataifa zinazohusika na masuala ya usafiri wa anga; na nne, kukosekana kwa taasisi ya kusimamia utekelezaji wa maamuzi wa Umoja wa Afrika yanayohusu usafiri wa anga.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa Katiba ya Tume ya mwaka 1969, Tanzania ilikabiliwa na changamoto zifuatazo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kukosekana kwa ushindani wa haki katika Mikataba ya Usafiri wa Anga nchini. Mfano, kutoruhusu makampuni mengine ya usafiri wa anga ikiwemo makampuni binafsi yenye umiliki wa asilimia 100 wawekezaji kutoka nje ya nchi kupewa leseni ya utoaji wa huduma za usafiri wa anga ili kutoa huduma za ndege zenye ratiba maalum kwa safari za nje ya nchi; pili, upungufu wa wataalam katika baadhi ya kada ikiwemo marubani, wahandisi wa matengenezo ya ndege na wataalam wa uchunguzi wa ajali za ndege; tatu, gharama kubwa za nauli za ndege kwa safari za ndani na nje ya nchi kutokana na masharti ya utoaji wa leseni za huduma za usafiri wa anga, pamoja na uwepo wa vikwazo vya wadhibiti wa idadi ya miruko ya ndege na idadi abiria katika safari ya ndege kwa wiki inayotokana na kutofungua soko huru la ndege nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, kutokuwepo kwa miongozo ya usafiri wa anga kwa nchi za Afrika kulikosababishwa na nchi wanachama ikiwemo Tanzania kushindwa kuwa na taratibu zinazoshabihiana katika usimamizi wa usafiri wa anga; na tano, Tanzania kushindwa kutekeleza maamuzi ya pamoja ya umoja wa Afrika yanayohusu usafiri wa anga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia chagamoto zilizoainishwa hapo juu, Umoja wa Afrika ulipendekeza kutungwa kwa Katiba Mpya ya Tume hiyo ya mwaka 2009. Kupitia Katiba mpya Umoja wa Afrika uliipatia Tume hiyo majukumu 16 kama yalivyooneshwa katika Ibara ya nne ya Katiba hiyo. Majukumu hayo mapya ni pamoja na yafuatayo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kufanya tafiti kuhusu udhibiti wa kitaalamu na maendeleo ya kiuchumi hasa katika kuimarisha usafiri wa anga Barani Afrika; pili, kusaidia nchi wanachama kufuata viwango vinavyopendekezwa na *ICAO* na mipango ya uongozaji ndege katika Afrika; tatu, kukuza na kuratibu miundombinu ya utoaji wa mafunzo na kuendeleza rasilimali watu katika tasnia ya usafiri wa anga; nne kuhamasisha na kusaidia katika uanzishaji mamlaka ya usafiri wa anga zinazojitegemea; tano, kuandaa mikakati ya pamoja ili kupata rasilimali ya kuwezesha usafiri wa anga wa kimataifa hususan mikakati ya uratibu wa ushirikiano wa nchi na nchi au nchi zaidi ya mbili kwa ajili ya ushirikiano wa kitaalamu kwa nchi wanachama.

Mheshimiwa Naibu Spika, sita kulinda maslahi ya nchi wanachama katika majukwaa ya kimataifa katika masuala yanayohusu usafiri wa anga; saba, kuhakikisha ushirikiano wa karibu wa Jumuiya ya Kikanda na mashirika mengine ya Afrika yanayohusu masuala ya anga; nane, kuandaa na kuainisha Sheria na Kanuni za usalama, utunzaji wa mazingira, ushindani wa haki, utatuzi wa migogoro kulinda haki za walaji na masuala mengine yanayohusu usafiri wa anga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 19 ya Katiba ya Tume ya mwaka 2009 iliweka sharti la Katiba hiyo kuanza kutekelezwa rasmi baada ya nchi 15 za Afrika kuridhia. Ilipofika tarehe 6 Aprili, 2021 nchi 15 kati ya nchi 55 za Afrika zilikuwa zimeridhia Katiba hiyo. Hivyo, ilianza kutekelezwa rasmi tarehe 6 Aprili, 2021. Kuanzia kipindi hicho, Tanzania ilikoma kuwa mwanachama wa Tume hiyo. Aidha, hadi sasa nchi 18 zimeridhia Katiba ya Tume hiyo ya 2009 kati ya nchi 41 zilizo-*sign*. Nchi zilizoridhia ni Angola, Kenya, Mali, Msumbiji, Burkina

Faso, Kongo, Gabon, Gambia, Niger, Siera Lione, Burundi, Cape Verde, Sudan, Togo, Senegal, Tunisia, na Rwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katiba ya Tume hiyo Mwaka 2009 ina majukumu ya Ibara ya 26 ama inajumuisha Ibara 26 maelezo ya Ibara hizo ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya kwanza inatoa tafsiri. Hii inaeleza kuhusu tafsiri ya maneno muhimu yaliyotumika katika Katiba hiyo. Ibara ya Pili, inazungumzia uanzishwaji wa Tume. Ibara hii inaelezea kuwa Tume iliyoanzishwa na Katiba ya mwaka 1969 itaendelea kuwepo na kutekeleza majukumu yake kama chombo cha Umoja wa Afrika kwa ajili ya masuala ya usafiri wa anga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya tatu na nne inazungumzia madhumuni ya Tume. Ibara hii inaeleza madhumuni ya kuanzishwa kwa Tume hiyo. Ibara ya tano, ni ya wanachama. Ibara hii inaeleza kuwa kila mwanachama atakuwa na haki sawa ya kushiriki na uwakilishi katika mikutano ya Tume hiyo. Ibara ya sita (Uwezo wa Kisheria). Ibara hii inaeleza kwamba Tume itatumia Sheria za nchi za mwanachama katika kutekeleza majukumu yake kwenye nchi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya saba (Upendeleo na Kinga). Ibara hii inaeleza kuwa Tume au Wawakilishi wa Tume na watumishi wake watakuwa na upendeleo wa kinga kwa mujibu wa Mkataba wa Upendeleo na Kinga wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika wa Mwaka 1964. Ibara ya nane (Makao Makuu). Ibara hii inaeleza kuwa Makao Makuu ya Tume yatakuwa Senegal na kwamba Makao Makuu hayo yanaweza kuhamishwa kadri itakavyoamuliwa na vikao vya wanachama wa Tume hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya tisa (Muundo wa Tume). Ibara hii inaeleza kuwa Muundo wa Tume utakuwa na Mkutano Mkuu Ofisi ya Usimamizi na sekretarieti. Ibara ya 10 (Mkutano Mkuu). Ibara hii inaeleza kuwa kutakuwa na Mkutano Mkuu ambao ndiyo utakuwa chombo Kikuu cha Maamuzi cha Tume. Ibara ya 11 (Kazi

za Mkutano Mkuu wa Wanachama). Ibara hii inaorodhesha kazi za Mkutano Mkuu wa Wanachama ikiwa ni pamoja na kutoa miongozo ya kisera, kuchagua Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti, kuidhinisha Muundo wa Tume na kuteua Katibu Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 12 (Ofisi ya Sekretarieti). Ibara hii inaeleza kuwa Ofisi ya Usimamizi wa Sekretarieti itakuwa na Rais na Makamu wa Rais watano watakaochanguliwa katika Mkutano kwa kuzingatia kanuni za uwakilishi wa kijiografia wa *AU;* Ibara ya 13 (Majukumu ya Ofisi ya Usimamizi wa Sekretarieti). Ibara hii inaeleza Majukumu ya Ofisi ya Usimamizi wa Sekretarieti ya Tume. Ibara ya 14 (Sekretarieti). Ibara hii inaeleza kuwa Sekretarieti ya Tume itaongozwa na Katibu Mkuu ambaye atachaguliwa na Mkutano Mkuu baada ya kupendekezwa na Ofisi ya Usimamizi wa Tume.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 15 (Wajibu wa Kutoa Taarifa). Ibara hii inaelekeza majukumu ya Kamati Ndogo ya Usafiri wa Anga ya Mawaziri wa nchi wanachama ambao itapokea na kuridhia mapendekezo ya Tume kuhusiana na masuala mbalimbali ya usafiri wa anga kwa kuzingatia taratibu za Umoja wa Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 16 (Ushirikiano na Taasisi Nyingine za Kimataifa). Ibara hii inaelezea kuwa Tume inatakiwa kufanya kazi kwa kushirikiana na Taasisi nyingine za *AU*, Taasisi za Kikanda, Shiririka la Usafiri wa Anga Duniani pamoja na Taasisi za Serikali na zisizo za Serikali zinazohusiana na utoaji wa huduma za usafiri wa anga. Ibara ya 17 (Vyanzo vya Mapato). Ibara hii inaeleza kuwa bajeti ya kawaida ya Tume itatokana na michango ya nchi wanachama. Bajeti ya nyongeza inaweza kuwepo ili kukidhi matumizi ya ziada au matumizi maalumu ya Tume.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 18 (Vikwazo). Ibara hii inaelekeza kuwa nchi wanachama itakayoshindwa kutoa michango ya uanachama kwa kipindi cha miaka miwili au zaidi itakuwa imepoteza haki ya kupiga kura kwenye Mkutano Mkuu au kutoa mgombea kwenye nafasi yoyote ya kuchaguliwa kwenye uongozi

wa Tume. Ibara ya 19 (Uwekaji Sahihi Kulipia na Kuanza Kutumika). Ibara hii inaeleza kuwa Katiba hii iko wazi kwa ajili ya kuwekewa saini na kuridhiwa na nchi za Afrika kwa kuzingatia utaratibu wa kikatiba wa kila nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 20 (Uanachama katika Kipindi cha Mpito). Ibara hii inaeleza kuwa bila kuadhiri ibara ya 26 nchi mwanachama chini ya Katiba ya Tume ya Mwaka 1969 itaendelea na uanachama wake wa Tume hadi pale Katiba ya mwaka 2009 itakapoanza kutumika. Ibara ya 24 (Lugha zitakazotumika). Ibara hii inafafanua kuwa lugha zitakazotumika katika utekelezaji wa majukumu ya Tume zitakuwa lugha zinazotumika na Umoja wa Afrika. Ibara ya 25 (Usajili). Ibara hii inaelezea kuwa Katiba ya Tume itasajiliwa na Shirika la Usafiri wa Anga Duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, manufaa ambayo Tanzania itayapata iwapo itaridhia Katiba ya Tume ya Mwaka 2009 ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kuendelea kufaidika na fursa za uongozi na ajira zinazojitokeza katika Tume hiyo; pili, kunufaika na matokeo ya tafiti zitakazofanyika kupitia Miongozo ya Tume; na tatu, Tanzania itaendelea kukidhi vya *ICAO* ikiwemo mipango ya uongozaji ndege.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe kuwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania ya Mwaka 1977 Ibara ya 63 (3) (e) nchi yetu imejiwekea utaratibu kuwa itifaki na mikataba yote ya kimataifa ambayo nchi yetu itatekeleza ni lazima iridhiwe na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hivyo, kutokana na utaratibu huo, Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi iliwasilisha mapendekezo haya mbele ya Bunge lako tukufu kwa ajili ya kuridhiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya awali, sasa naomba kuwasilisha mapendekezo ya kuridhia Azimio la Katiba

ya Tume ya Usafiri wa Anga ya Afrika ya Mwaka 2009 kama ifuatavyo: -

KWA KUWA, Jamhuri Ya Muungano wa Tanzania ni miongoni mwa nchi wanachama wa Umoja wa afrika ulioanzishwa mnamo tarehe 11 Julai, 2000 kupitia Mkataba wa Uanzishwaji wa Umoja wa Afrika ukichukua nafasi ya uliokuwa Umoja wa Nchi huru za Afrika *(Organization for African Union – OAU);*

Na kwa kuwa, katika juhudi za kuimarisha ushirikiano na kukabiliana na chanagamoto mbalimbali za kisekta zilizokuwa zikikabili Bara la Afrika kwa wakati huo, nchi wanachama waliokuwa wanachama wa nchi huru za Afrika ikiwemo Tanzania, zilisaini mikataba na hati mbalimbali ikiwemo hati ya kuanzisha Katiba ya Tume ya Usafiri wa Anga ya Afrika ya Mwaka 1969 ambayo ilianzisha Tume ya Usafiri ya Anga ya Afrika kwa lengo la kukabiliana na changamoto mbalimbali za sekta ya Usafiri wa Anga pamoja na kuimarisha na kuboresha huduma za Usafiri wa Anga katika Bara la Afrika;

Na kwa kuwa, kuanzishwa kwa Katiba ya Tume ya Usafiri wa Anga ya Afrika na Tume ya Usafiri wa Anga wa Afrika kulileta mafanikio mbalimbali yaliyokuwemo ya kuwezesha mamlaka ya Usafiri wa Anga wa za nchi wanachama kuwa na utaratibu wa kujadili na kupanga kwa pamoja hatua zote zinazohitajia katika uratibu na ushirikiano wa shughuli za usafiri wa anga, kusaidia kukuza matumizi bora na uendelezaji wa mifumo ya usafiri wa anga katika nchi wanachama, na kuwezesha wanachama kuwa na taasisi ya pamoja ya kuratibu masuala ya usafiri wa anga;

Na kwa kuwa, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, tangu kuanzishwa kwa Katiba ya Tume ya Usafiri wa Anga ya Afrika na Tume ya Usafiri wa Anga ya Afrika, changamoto mbalimbali zilibainika zikiwemo kukosekana kwa Taasisi ya kusimamia utekelezaji wa maamuzi kuhusu ulegezaji wa masharti ya usafiri wa anga Barani Afrika, kutokuwepo kwa Sheria na Kanuni zinazosimamia ushindani

wa biashara ya usafiri wa anga zinazotoa fursa na usawa kwa wadau pamoja na kukuza ushindani katika nchi wanachama;

Na kwa kuwa, ili kukabiliana na changamoto zilizobainika mnamo tarehe 16 Desemba, 2009, nchi wanachama wa Umoja wa Afrika zilipitisha Katiba ya Tume ya Usafiri wa Anga ya Mwaka 2009 ambayo ilianza kutumika tarehe 9 Januari, 2020;

Na kwa kuwa, Katiba mpya ya Tume ya Usafiri wa Anga ya Afrika ya mwaka 2009 imefuta Katiba ya Tume ya Usafiri wa Anga ya Afrika ya mwaka 1969 iliyoridhiwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 26 Septemba, 1969 na hivyo kwa sasa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania siyo nchi mwanachama wa Tume ya Usafiri wa Anga ya Afrika kwa kuwa haijaridhia Katiba mpya ya mwaka 2009;

Na kwa kuwa, kwa kuzingatia manufaa mbalimbali ambayo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliwapata kwa kuridhia Katiba iliyofutwa ya Tume ya Usafiri wa Anga ya Mwaka 1969 kuridhiwa kwa Katiba mpya ya Tume ya Usafiri wa Anga ya Afrika ya Mwaka 2009 kutaleta manufaa mbalimbali kwa Jamhuri ya Muungano kama yafuatayo: -

(1) Kuimarika kwa usalama katika masuala ya usafiri wa anga hapa nchini;

(2) Kuongezeka kwa ufanisi katika utoaji wa huduma za usafiri wa anga kutokana na mafunzo yanayotolewa na yatakayoendelea kutolewa na Taasisi za kimataifa kupitia Tume hiyo;

(3) Kuongezeka kwa ufanisi wa uongozi, mafunzo, kuongezeka kwa fursa za uongozi, mafunzo, ajira na utafiti zinazotolewa au kuratibiwa na tume hiyo; na

(4) Kuongeza wigo wa ushiriki wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika masuala yanayohusu usafiri wa anga katika nyanja ya kimataifa.

Hivyo basi, kwa kuzingatia manufaa hayo ambayo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itaipata kutokana na kuridhia Katiba Mpya ya Tume ya Usafiri wa Anga ya Afrika ya Mwaka 2009, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wake wa Kumi na Mbili, na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, ninaazimia kuridhia Katiba mpya ya Tume ya Usafiri wa Anga ya Afrika ya mwaka 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa, naomba kutoa hoja.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Mwenyekiti wa Kamati.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, yafuatayo ni maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Azimio la Bunge kuridhia Katiba ya Tume ya Usafiri wa Anga ya Afrika ya mwaka 2009, *The Constitution of The African Civil Aviation Commission 2009.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Maoni ya Kamati, Utangulizi. Maelezo ya Awali; kwa mujibu wa Kanuni ya 60(b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu Kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Katiba ya Tume ya Usafiri wa Anga ya mwaka 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, namna Kamati Ilivyotekeleza Kazi; baada ya kupokea maelekezo yako ya kulishughulikia jambo hili kwa mujibu wa Kanuni ya 108, Kamati ilifanya yafuatayo: -

a) Kufanya uchambuzi wa awali ambapo Wajumbe walipata fursa ya kujadili masuala muhimu yanayojitokeza katika Mapendekezo ya Azimio la Kuridhia Katiba hiyo;

b) Kupokea na kujadili Maelezo ya Serikali kuhusu Mapendekezo ya Azimio la Kuridhia Katiba, ambayo yaliwasilishwa na Mhe. Atupele Fredy Mwakibete (Mb), Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi) siku ya Jumanne tarehe 22 Agosti, 2023;

c) Kupokea na kuchambua Maoni ya Wadau yaliyowasilishwa kwa njia ya mtandao ambapo taasisi moja iliwasilisha maoni yake; na

d) Kufanya majumuisho ya Serikali kuhusu hoja mbalimbali zilizobainika katika uchambuzi uliofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, Kamati ilifanya tathimini kwa kuzingatia Kanuni ya 107(2)(f) na (g) ili kupima iwapo kuna manufaa au athari ambazo Tanzania itapata kutokana na mapendekezo ya Serikali kwa Bunge kuridhia Katiba husika. Tathimini iliyofanyika ilikuwa na lengo la kuhakikisha kwamba Katiba inayopendekezwa kuridhiwa kwa Azimio la Bunge inachangia kukuza ushirikiano, usalama, na maendeleo ya usafiri wa anga baina ya Tanzania na nchi nyingine katika Bara la Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uchambuzi wa Kamati, Chimbuko; Tume ya Usafiri wa Anga ya Afrika *(AFCAC)* ni Shirika la Kimataifa lililoanzishwa kwa lengo la kukuza na kuratibu shughuli za usafiri wa anga Barani Afrika. Tume hii ilianzishwa baada ya Mkutano ulioitishwa na Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga *(ICAO)* na lililokuwa Shirikisho la Umoja wa Afrika *(OAU)* mwaka 1969, uliofanyika mjini Addis Ababa nchini Ethiopia. Baada ya kuanzishwa

kwake, shirika lilipata hadhi rasmi na kuwa Wakala Maalum wa Umoja wa Afrika *(OAU)* mwaka 1978.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katiba ya Tume ya Usafiri wa Anga ya Afrika ilipitishwa mwaka 1969 na kuridhiwa na Tanzania tarehe 26 Septemba, 1969. Aidha, katiba hiyo ilianza kutumika rasmi mwaka 1972 kwa nchi zote ambazo ziliridhia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo mwaka 2009 nchi wanachama wa *AFCAC* zilipitisha Katiba mpya ambayo ilifuta Katiba ya awali kwa lengo la kutoa mfumo ulioboreshwa wa kisheria katika shughuli za usafiri wa anga barani Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu za kufutwa kwa Katiba ya awali ni kutokana na kubainika kwa changamoto mbalimbali zikiwemo zifuatazo: -

i. Kukosekana kwa taasisi ya kusimamia utekelezaji wa maamuzi ya Tume kuhusu ulegezaji wa masharti ya usafiri wa anga baina ya nchi wanachama pamoja na maamuzi ya Umoja wa Afrika *(AU)* yanayohusu sekta ya anga;

ii. Kutokuwepo kwa mfumo wa kisheria ambao unasimamia ushindani wa kibiashara baina ya nchi wanachama; na

iii. Kutokuwepo kwa uhusiano wa kisera unaoridhisha baina ya nchi wanachama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mapendekezo ya Katiba Mpya ya Mwaka 2009 Serikali imewasilisha hoja ili kwamba Bunge likubali kuridhia Katiba ya Tume ya Usafiri wa Anga wa Afrika ya mwaka 2009 *(The Constitution of the African Civil Aviation Commission, 2009)*. Katiba hiyo ilitungwa ili kutatua changamoto za utekelezaji na mapungufu yaliyobainika katika Katiba ya mwaka 1969.

Mheshimiwa Naibu Spika, katiba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge lako tukufu imeanzisha muundo wa kisasa wa Tume ya *AFCAC* na kubainisha majukumu kulingana na mabadiliko katika sekta ya usafiri wa anga kwa kuzingatia mahitaji ya Afrika. Aidha, Katiba inajibu hoja mbalimbali zilizotokana na mabadiliko ya mara kwa mara katika usafiri wa anga kimataifa na kikanda, na pia inatatua changamoto za utekelezaji wa Katiba ya Mwaka 1969.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Katiba iliyopendekezwa kuridhiwa, Tume imekabidhiwa majukumu mbalimbali yakiwemo yafuatayo: -

i. Kusaidia Nchi Wanachama kufuata viwango pendekezwa vya Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga *(ICAO),* na mipango ya uongozaji ndege katika Bara la Afrika;

ii. Kulinda masilahi ya nchi wanachama katika majukwaa ya kimataifa katika masuala yanayohusu usafiri wa anga; na

iii. Kuandaa na kuwianisha Sheria na Kanuni za usalama, utunzaji wa mazingira, ushindani wa haki, utatuzi wa migogoro, kulinda haki za walaji na masuala mengineyo yanayohusu usafiri wa anga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maudhui ya Katiba Mpya; Katiba inayopendekezwa kuridhiwa ina ibara 26 ambazo kwa ujumla wake zimejikita katika maudhui yenye lengo la: -

i. Kuendelea kuitambua na kuiwekea majukumu Tume ya Usafiri wa Anga ya Africa *(AFCAC),* ikiwemo kubainisha muundo wake na uwezo wake kisheria;

ii. Kuainisha haki, wajibu wa wanachama wa *AFCAC* ikiwemo kuhudhuria mkutano mkuu, kulipa michango ya uanachama na haki ya kujitoa uanachama;

iii. Kubainisha ushirikiano baina ya *AFCAC* na taasisi nyingine za kikanda na za kimataifa zinazojihusisha na utoaji wa huduma ya usafiri wa anga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa mchakato wa kuridhia katiba mpya; baada ya kutungwa Katiba ya mwaka 2009, utekelezaji wa masharti ya Katiba hiyo ulianza rasmi tarehe 6 Aprili, 2021. Hadi kufikia tarehe 31 Oktoba, 2022 nchi 41 kati ya nchi 55 wanachama wa Umoja wa Afrika zilikuwa zimesaini; na hadi kufikia tarehe 31 Oktoba, 2022 nchi 18 kati ya nchi 41 zilizosaini zilikuwa zimeridhia Katiba Mpya. Nchi hizo ni: Angola, Burkina Faso, Burundi, Cape Verde, Congo, Eswatini, Gambia, Gabon, Kenya, Mali, Msumbiji, Niger, Rwanda, Senegal, Sierra Leone, Sudan, Togo, na Tunisia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katiba inayopendekezwa kuridhia, imeweka bayana sharti katika Ibara ya 19 kwamba, kila nchi mwanachama ina uhuru wa kutia saini na kuridhia kwa utaratibu ulioainishwa katika mifumo ya kisheria ya nchi husika. Kwa muktadha huo, Tanzania inaweza kuridhia katiba hiyo kwa mujibu wa masharti yaliyoainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imebaini kwamba tangu katiba mpya ianze kutekelezwa rasmi tarehe 6 Aprili, 2021, Tanzania ilikuwa haijaridhia, na kwa kutofanya hivyo tumeshindwa kutekeleza maamuzi ya pamoja ya Umoja wa Afrika yanayohusu usafiri wa anga. Aidha, kwa kutoridhia kunaifanya Tanzania kutokuwa na miongozo stahiki ya usafiri wa anga itokanayo na maamuzi hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maoni na Ushauri wa Kamati; baada ya kuchambua Hoja ya Serikali kuhusu Azimio la Kuridhia Katiba ya Tume ya Usafiri wa Anga ya Afrika ya mwaka 2009 *(The Constitution of The African Civil Aviation Commission, 2009)*, Kamati ina maoni na ushauri ufuatao: -

a) Bunge liridhie Katiba hii kwa kuzingatia umuhimu wake katika utekelezaji wa malengo ya kitaifa na kimataifa katika kuleta ufanisi na ubora wa sekta ya usafiri wa anga, pamoja na uhusiano wa kidiplomasia baina ya nchi wanachama;

b) Serikali ichangamkie fursa ya kuendelea kutangaza lugha ya Kiswahili kupitia vikao mbalimbali vya Tume na kuhamaisha Watanzania kuchangamkia fursa za ajira katika Tume hiyo;

c) Serikali kuwa mstari wa mbele kuhakikisha kwamba Tanzania inanufaika kikamilifu na soko huru la usafiri wa anga barani Afrika, na kushiriki kikamilifu katika kuandaa sheria na kanuni za kuwezesha ushindani endelevu;

d) Serikali ihakikishe inatekeleza wajibu wake katika kuboresha maudhui ya katiba na kupendekeza kwa Tume, marekebisho ya katiba ili kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa malengo ya Tume; na

e) Serikali kuendelea kuwashirikisha wadau muhimu na sekta binafsi katika maboresho ya utendaji wa sekta ya anga ndani ya nchi na kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hitimisho; naomba nitumie fursa hii kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Spika na wewe binafsi kwa kuliongoza vema Bunge hili na kwa namna ambavyo mmeipa Kamati ushirikiano. Ushauri wako na maelekezo yako vimekuwa ni nyenzo muhimu katika ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu ambao walitoa maoni mbalimbali kwa lengo la kuboresha maudhui ya Azimio la kuridhia katiba hii. Kwa kutambua mchango wao, naomba majina yao yaingie katika Taarifa Rasmi za Bunge kama ilivyoainishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mhe. Prof. Makame Mnyaa Mbarawa (Mb) Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, akisaidiwa na Mhe. Atupele Fredy Mwakibete, Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi) kwa ushirikiano ambao wameipatia Kamati katika kipindi chote cha uchambuzi wa Azimio hili. Aidha, nawashukuru watendaji wote wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi na Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania *(TCAA)* chini ya uongozi wa Katibu Mkuu (Sekta ya Uchukuzi) Bw. Gabriel J. Migire kwa kutoa maelekezo ya kitaalam na ufafanuzi pale walipohitajika kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini sio kwa umuhimu, niwashukuru Watumishi wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge, Ndg. Nenelwa J. Mwihambi, *ndc*, kwa uratibu wa shughuli za Kamati, kutoa ushauri wa kitaalam wakati wa uchambuzi wa awali wa mapendekezo ya kuridhia Katiba hii hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uamuzi Kuhusu Hoja; kwa mamlaka ambayo Bunge limepewa kwa mujibu wa Ibara ya 63(3) (e)ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, naomba sasa Bunge lijadili na kuridhia Katiba ya Tume ya Usafiri wa Anga ya Afrika ya mwaka 2009 *(The Constitution of The African Civil Aviation Commission, 2009)* Kama Ilivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha, na ninaunga mkono hoja.

**MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU KUHUSU AZIMIO LA BUNGE KURIDHIA KATIBA YA TUME YA USAFIRI WA ANGA YA AFRIKA YA MWAKA 2009 *(THE CONSTITUTION OF THE AFRICAN CIVIL AVIATION COMMISSION, 2009)* – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

**1.0 UTANGULIZI**

1.1 **Maelezo ya Awali**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 60 (6) (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha **Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu Kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Katiba ya Tume ya Usafiri wa Anga ya Mwaka 2009** *(The Constitution of the African Civil Aviation Commission, 2009)*.

1.2 **Namna Kamati Ilivyotekeleza Kazi**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kupokea maelekezo yako ya kulishughulikia jambo hili kwa mujibu wa **Kanuni ya 108**, Kamati ilifanya yafuatayo: -

a) Kufanya uchambuzi wa awali ambapo Wajumbe walipata fursa ya kujadili masuala muhimu yanayojitokeza katika Mapendekezo ya Azimio la Kuridhia Katiba hiyo;

b) Kupokea na kujadili Maelezo ya Serikali kuhusu Mapendekezo ya Azimio la Kuridhia Katiba, ambayo yaliwasilishwa na Mhe. Atupele Fredy Mwakibete (Mb), Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi) siku ya Jumanne tarehe 22 Agosti, 2023;

c) Kupokea na kuchambua Maoni ya Wadau yaliyowasilishwa kwa njia ya mtandao ambapo taasisi moja (1) iliwasilisha maoni yake; na

d) Kufanya majumuisho na Serikali kuhusu hoja mbalimbali zilizobainika katika uchambuzi uliofanyika.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na hayo, Kamati ilifanya tathimini kwa kuzingatia Kanuni ya 107 (2) (f) na (g) ili kupima iwapo kuna manufaa au athari ambazo Tanzania itapata kutokana na mapendekezo ya Serikali kwa Bunge kuridhia Katiba husika. Tathimini iliyofanyika ilikuwa na lengo la kuhakikisha kwamba Katiba inayopendekezwa kuridhiwa kwa Azimio la Bunge inachangia kukuza ushirikiano, usalama, na maendeleo ya usafiri wa anga baina ya Tanzania na nchi nyingine katika Bara la Afrika.

**2.0 UCHAMBUZI WA KAMATI**

2.1 **Chimbuko**

**Mheshimiwa Spika**, Tume ya Usafiri wa Anga ya Afrika (AFCAC) ni Shirika la Kimataifa lililoanzishwa kwa lengo la kukuza na kuratibu shughuli za usafiri wa anga barani Afrika. Tume hii ilianzishwa baada ya Mkutano ulioitishwa na Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga (ICAO) na lililokuwa Shirikisho la Umoja wa Afrika (OAU) Mwaka 1969, Addis Ababa nchini Ethiopia. Baada ya kuanzishwa kwake, shirika lilipata hadhi rasmi ya kuwa Wakala Maalum wa Umoja wa Afrika (OAU) Mwaka 1978.

**Mheshimiwa Spika**, Katiba ya Tume ya Usafiri wa Anga ya Afrika ilipitishwa mwaka 1969 na kuridhiwa na Tanzania tarehe 26 Septemba, 1969. Aidha, Katiba hiyo ilianza kutumika rasmi mwaka 1972 kwa nchi zote ambazo ziliridhia.

**Mheshimiwa Spika**, mnamo mwaka 2009 nchi wanachama wa AFCAC zilipitisha Katiba mpya ambayo ilifuta Katiba ya awali kwa lengo la kutoa mfumo ulioboreshwa wa kisheria katika shughuli za usafiri wa anga barani Afrika.

**Mheshimiwa Spika**, sababu za kufutwa kwa Katiba ya awali ni kutokana na kubainika kwa changamoto mbalimbali zikiwemo zifuatazo: -

a) Kukosekana kwa taasisi ya kusimamia utekelezaji wa maamuzi ya Tume kuhusu ulegezaji wa masharti ya usafiri wa anga baina ya nchi wanachama Pamoja na maamuzi ya Umoja wa Afrika (AU) yanayohusu Sekta ya Anga;

b) Kutokuwepo kwa mfumo wa kisheria ambao unasimamia ushindani wa kibiashara baina ya nchi wanachama; na

c) Kutokuwepo kwa uhusiano wa kisera unaoridhisha baina ya nchi wanachama.

2.2 **Mapendekezo ya Katiba Mpya ya Mwaka 2009**
**Mheshimiwa Spika**, Serikali imewasilisha hoja ili kwamba Bunge likubali kuridhia Katiba ya Tume ya Usafiri wa Anga wa Afrika ya Mwaka 2009 *(The Constitution of the African Civil Aviation Commission, 2009)*. Katiba hiyo ilitungwa ili kutatua changamoto za utekelezaji na mapungufu yaliyobainika katika Katiba ya Mwaka 1969.

**Mheshimiwa Spika,** Katiba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge lako tukufu imeanzisha muundo wa kisasa wa Tume (AFCAC) na kubainisha majukumu kulingana na mabadiliko katika sekta ya usafiri wa anga kwa kuzingatia mahitaji ya Afrika. Aidha, Katiba inajibu hoja mbalimbali zilizotokana na mabadiliko ya mara kwa mara katika usafiri wa anga kimataifa na kikandani, na pia inatatua changamoto za utekelezaji wa Katiba ya Mwaka 1969.

**Mheshimiwa Spika**, kupitia Katiba inayopendekezwa kuridhiwa, Tume imekabidhiwa majukumu mbalimbali yakiwemo yafuatayo: -

a) Kusaidia Nchi Wanachama kufuata viwango pendekezwa vya Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga (ICAO), na mipango ya uongozaji ndege katika Bara la Afrika;

b) Kulinda masilahi ya Nchi Wanachama katika majukwaa ya kimataifa katika masuala yanayohusu usafiri wa anga; na

c) Kuandaa na kuwianisha Sheria na Kanuni za usalama, utunzaji wa mazingira, ushindani wa haki, utatuzi wa migogoro, kulinda haki za walaki na masuala mengineyo yanayohusu usafiri wa anga.

2.3 **Maudhui ya Katiba Mpya**
**Mheshimiwa Spika**, Katiba inayopendekezwa kuridhiwa ina ibara 26 ambazo kwa ujumla wake zimejikita katika maudhui yenye lengo la:-

a) Kuendelea kuitambua na kuiwekea majukumu Tume ya Usafiri wa Anga ya Africa (AFCAC), ikiwemo kubainisha muundo wake na uwezo wake kisheria;

b) Kuainisha haki, wajibu wa Wanachama wa AFCAC ikiwemo kuhudhuria Mkutano Mkuu, kulipa michango ya uanachama na haki ya kujitoa uanachama ;

c) Kubainisha ushirikiano baina ya AFCAC na taasisi nyingine za kikanda na za kimataifa zinazojihusisha na utoaji wa huduma za usafiri wa anga.

2.4 **Mchakato wa Kuridhia Katiba Mpya**
**Mheshimiwa Spika**, baada ya kutungwa Katiba ya Mwaka 2009, utekelezaji wa masharti ya Katiba hiyo ulianza rasmi tarehe 6 Aprili, 2021. Hadi kufikia tarehe 31 Oktoba 2022 nchi 41 kati ya nchi 55 wanachama wa Umoja wa Afrika zilikuwa zimesaini na hadi kufikia tarehe 31 Oktoba, 2022 nchi 18 kati ya nchi 41 zilizosaini zilikuwa zimeridhia Katiba Mpya. Nchi hizo ni: **Angola**, **Burkina Faso**, **Burundi**, **Cape Verde**, **Congo**, **Eswatini**, **Gambia**, **Gabon**, **Kenya**, **Mali**, **Msumbiji**, **Niger**, **Rwanda**, **Senegal**, **Sierra Leone**, **Sudan**, **Togo**, na **Tunisia**.

**Mheshimiwa Spika**, Katiba inayopendekezwa kuridhia, imeweka bayana sharti katika Ibara ya 19 kwamba, kila nchi mwanachama ina uhuru wa kutia saini na kuridhia kwa utaratibu ulioainishwa katika mifumo ya kisheria ya nchi husika. Kwa muktadha huo, Tanzania inaweza kuridhia Katiba hiyo kwa mujibu wa masharti yaliyoainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ya Mwaka 1977.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kwamba tangu Katiba Mpya ianze kutekelezwa rasmi tarehe 6 Aprili, 2021, Tanzania ilikuwa

haijaridhia na kwa kutofanya hivyo, tumeshindwa kutekeleza maamuzi ya Pamoja ya Umoja wa Afrika yanayohusu usafiri wa anga. Aidha, kwa kutoridhia kunaifanya Tanzania kutokuwa na miongozo stahiki ya usafiri wa anga itokanayo na mamuzi hayo.

**3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kuchambua Hoja ya Serikali kuhusu Azimio la Kuridhia **Katiba ya Tume ya Usafiri wa Anga ya Afrika Ya Mwaka 2009** *(The Constitution of The African Civil Aviation Commission, 2009)*, Kamati ina maoni na ushauri ufuatao: -

a) Bunge liridhie Katiba hii kwa kuzingatia umuhimu wake katika utekelezaji wa malengo ya kitaifa na kimataifa katika kuleta ufanisi na ubora wa sekta ya usafiri wa anga, pamoja na uhusiano wa kidiplomasia baina ya nchi wanachama;

b) Serikali ichangamkie fursa ya kuendelea kutangaza Lugha ya Kiswahili kupitia vikao mbalimbali vya Tume na kuhamaisha Watanzania kuchangamkia fursa za ajira katika Tume hiyo;

c) Serikali kuwa mstari wa mbele kuhakikisha kwamba Tanzania inanufaika kikamilifu na soko huru la usafiri wa anga barani Afrika, na kushiriki kikamilifu katika kuandaa sheria na kanuni za kuwezesha ushindani endelevu;

d) Serikali ihakikishe inatekeleza wajibu wake katika kuboresha maudhui ya Katiba kwa kupendekeza kwa Tume, marekebisho ya Katiba ili kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa malengo ya Tume; na

e) Serikali kuendelea kuwashirikisha wadau muhimu na sekta binafsi katika maboresho ya utendaji wa sekta ya anga ndani ya nchi na kimataifa.

**4.0 HITIMISHO**

4.1 **Shukrani**

**Mheshimiwa Spika**, naomba nitumie fursa hii kukushukuru kwa dhati wewe binafsi, ukisaidiwa na Naibu Spika kwa kuliongoza vema

Bunge hili na kwa namna ambavyo umeipa Kamati ushirikiano. Ushauri wako na maelekezo yako vimekuwa ni nyenzo muhimu katika ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu.

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu ambao katika kutekeleza majukumu yao kikanuni, walichambua, kujadili, na kutoa maoni mbalimbali kwa lengo la kuboresha maudhui ya Azimio la kuridhia Katiba hii. Kwa kutambua mchango wao, naomba majina yao yaingie katika Taarifa Rasmi za Bunge kama ifuatavyo: -

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Moshi Selemani Kakoso, Mb. | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Anne Kilango Malecela, Mb. | Makamu Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Abdallah Jafari Chaurembo, Mb. | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Abubakar Damian Asenga, Mb. | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Ahmed Mabkhut Shabiby, Mb. | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Ally Anyigulile Mlaghila Jumbe,Mb. | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Amina Ali Mzee, Mb. | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Angelina Adam Malembeka, Mb. | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Kapt. Abbas Ali Hassan Mwinyi,mb. | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Eng. Mwanaisha Ng'anzi Ulenge, Mb. | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Fredrick Edward Lowassa, Mb. | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Ghati Zephania Chomete, Mb. | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Innocent Edward Kalogeris, Mb. | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Livingstone Lusinde, Mb. | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Mbarouk Juma Khatib, Mb. | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Miraji Jumanne Mtaturu, Mb. | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Mohamed Maulid Ali, Mb. | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Mwatum Dau Haji, Mb. | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Rose Vicent Busiga, Mb. | Mjumbe |
| 20. | Mhe. Santiel Eric Kirumba, Mb. | Mjumbe |
| 21. | Mhe. Stella Simo n Fiyao, Mb. | Mjumbe |
| 22. | Mhe. Sylvia Francis Sigula, Mb. | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika**, namshukuru Mhe. Prof. Makame Mnyaa Mbarawa (Mb.) – Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, akisaidiwa na Mhe.

Atupele Fredy Mwakibete, Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi) kwa ushirikiano ambao wameipatia Kamati katika kipindi chote cha uchambuzi wa Azimio hili. Aidha, nawashukuru watendaji wote wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi na Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) chini ya uongozi wa Katibu Mkuu (Sekta ya Uchukuzi) Bw. Gabriel J. Migire kwa kutoa maelezo ya kitaalam na ufafanuzi pale walipohitajika kufanya hivyo.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini sio kwa umuhimu, niwashukuru Watumishi wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge, Ndg. Nenelwa J. Mwihambi, *ndc*, kwa uratibu wa shughuli za Kamati, kutoa ushauri wa kitaalam wakati wa uchambuzi wa awali wa mapendekezo ya kuridhia Katiba hii hadi kukamilika kwa taarifa hii.

4.2 **Uamuzi Kuhusu Hoja**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mamlaka ambayo Bung limepewa kwa mujibu wa Ibara ya 63 (3) (e)ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ya Mwaka 1977, naomba sasa Bunge lijadili na kuridhia **KATIBA YA TUME YA USAFIRI WA ANGA YA AFRIKA YA MWAKA 2009** *(THE CONSTITUTION OF THE AFRICAN CIVIL AVIATION COMMISSION, 2009)* kama ilivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha, na ninaunga mkono Hoja.

Moshi Selemani Kakoso, Mb.
**MWENYEKITI**
**Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu**
Agosti, 2023

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati, ahsante sana. Sasa tunaanza michango na kujadili. Tunaanza na Mheshimiwa Chamuriho wajiandae Waheshimiwa Ally Jumbe Mlaghila, Mheshimiwa Asenga, Mheshimiwa Kalogeris na Mheshimiwa Stella Simon Fiyao.

**MHE. ENG. DKT. LEONARD M. CHAMURIHO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniruhusu kuwa mchangiaji wa kwanza kwenye suala hili. Huu mkataba ni mzuri kwa *AU* kwa maudhui yake na utakwenda kutoa fursa nyingi kama ambavyo imetamkwa kuhusu faida zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna masuala ambayo yamo ndani ya hii itifaki ya kuridhia ambayo hayakuelezwa sawasawa, ambazo ni changamoto tunazoweza kuzipata katika kutekeleza hiki kitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nitajikita kwenye Mkataba wa *Yamoussoukro* ambao umeongelewa katika itifaki hii, ambao maudhui yake ni kufungua usafiri wa anga kwa Afrika nzima. Huko nyuma tuliona kwamba hili ni jambo jema lakini kwa mataifa ambayo yana mashirika ya ndege machanga inakuwa ni changamoto kidogo na ni hatari.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii *Yamoussoukro Decision* kama ambavyo imeonekana kwenye hii itifaki, tulikubaliana mwaka 1999 lakini bado sisi tulikuwa hatujaridhia kuitekeleza. Tulisaini lakini hatujaridhia kwa sababu ya athari zake ambazo tuliziona kule nyuma, ilikuwa ni kwamba, tunapokuwa na shirika dogo linaloanza tukifungua anga moja kwa moja, mashirika makubwa yatatumeza na tutashindwa kukua kwa haraka. Tulikuwa tunaona kwamba tungepata muda fulani ili tuweze kukua ili tuweze kuingia katika ushindani huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maelezo yaliyotolewa sikupata hiyo *comfort* kwamba kuna muda fulani ambao tutajizatiti katika kujenga uwezo wa shirika letu la ndege ili tusimezwe na mashirika makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa *Yamoussoukro Decision*, una maana kwamba mashirika ya nje kwa mfano yanaweza yakapita ndani yakachukua abiria katika vituo vyetu vya

ndani. Hiyo inafaa kwa nchi ambayo haina shirika la ndege, lakini kama una shirika lako la ndege inakuwa ni changamoto kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukienda katika kifungu cha tatu ambacho ni *objectives,* yaani malengo. Nikiangalia kifungu cha 3 (b) nikisoma kama kilivyoandikwa ni *"Facilitating, coordinating and ensuring their successful implementation of Yamoussoukro Decision by supervising and managing African liberalise Air Transport Industry*". Hapa ndipo penye changamoto. Tukishachukua tungeambiwa vizuri kwamba tumejipangaje katika kulinda shirika letu la ndege lisimezwe wakati linakua.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, nikiangalia *Article No.* 4 (j) ambayo inasema, katika kazi mojawapo nikisoma hapa kama ilivyoandikwa ni "*Pursuant to provision of the Article* 9 *of the Yamoussoukro Decision to discharge the duty of the executing agency of air transport in Africa*". Kwa hiyo bado tunasukuma kwamba, kama lengo litakuwa ni kusukuma utekelezaji wa hii *Yamoussoukro Decision*.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nikiangalia *Article 11 (i) function of the plenary* nayenyewe inaonesha kwamba itahakikisha utekelezaji wa hiyo *Yamoussoukro Decision*. Pia nikiangalia *Article* 18 ambayo inaongelea vikwazo ambavyo unaweza kufanyiwa. Kuna vikwazo ambavyo tunaweza tukawekewa kama tutashindwa utekelezaji wa hiyo kitu. Kwahiyo, ina maana kama tukishakubaliana na ile halafu tukasema anga linafunguliwa, huwezi kulizuia shirika la ndege la nchi nyingine, kwa mfano kupita Dar es Salaam likachukua abiria likawateremsha *KIA* au Mwanza na ambapo hiyo ilikuwa ni majukumu ya mashirika yetu ya ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tungepata maelezo mafupi tujue kwamba katika kuridhia hii, je, ulinzi wa shirika letu dogo ambalo linakua litakuwaje na tumechukulia vipi? Kwa hali ilivyo na bado tunakua; nilikuwa nashauri kwamba, tuweke muda wa kuruhusu shirika letu kukua kabla ya kuingia katika huu mradi ambao

utahusisha ku-*liberalise Air Transport Industry* kwani katika ukuaji huo tunaweza tukamezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asenga, jiandae Mheshimiwa Kalogeris.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi nami niweze kuchangia hoja iliyoko mezani. Mimi kama mjumbe wa Kamati ya Miundombinu kwa kweli tulipata nafasi nzuri ya kupitia hoja hii na naunga mkono hoja ili turidhie Katiba ya Tume ya Usafiri wa Anga ya Mwaka 2009 kwa sababu faida ni nyingi kuliko hasara, na nchi yetu si kisiwa useme kwamba kuna baadhi ya vitu tunaweza kujitenga navyo, japokuwa watu wanaweza kuwa waogawaoga na mambo haya ya maridhiano. Mimi nataka kuchangia maeneo kama matatu au manne.

Mheshimiwa Naibu Spika, chini ya Shirika la Usafiri wa Anga *ICAO* na wa *OAU* kama Mheshimiwa Waziri na Mwenyekiti wa Kamati walivyowasilisha hapa, Tanzania tuliridhia ile ya mwaka 1969 na kwa mujibu wa Katiba hii mpya ya 2009 ni wazi kwa kile kipengele ambacho kinasema kwamba nchi 15 zikisha saini utekelezaji unaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi Tanzania tumeshaanza kusukumwa nje kwa sababu nchi 41 tayari zimeshasaini maridhiano haya na wenzetu wanaanza kunufaika kuliko sisi. Hata huko nyuma tulishawahi kupata hadi fedha za uwekezaji kwenye mambo ya ushirikiano wa usafiri wa anga.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakupa mfano mmoja, mimi na baadhi ya Wabunge wenzangu tulisafiri hapa na Timu ya Wananchi tukaenda katika nchi mojawapo. Tukiwa na ile Timu ya Wananchi pamoja na Waheshimiwa na wanashabiki wengine wa hiyo timu katika nchi hiyo, tulivyotua pale *airport* tulitumia kama masaa

matatu hivi, bila ya kujali hawa ni Wabunge ama sio Waheshimiwa Wabunge na viongozi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mlolongo ulikuwa mkubwa sana. Sasa hatukufahamu kitu, baadaye katika upelelezi nitaeleza umuhimu wa maridhiano haya, tukawa tunaangalia wale watu wanaotuhudumia pale kama kuna wengine ni wanachama labda wa timu nyingine pinzani na sisi hata katika nchi yetu ama katika nchi ile nyingine na kujiuliza kwa nini tunapata usumbufu wa namna hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, tukajua, mojawapo ya sababu ni kwamba nchi hiyo tuliokwenda sisi hatukuwepo kwenye maridhiano ya pamoja ya anga. Kama tungekwenda katika nchi nyingine ina maana tungenufaika, tungefika pale wangeambiwa kuna Watanzania 50 wanakuja katika nchi yetu. Tungepokelewa vizuri, tungepita na ule usumbufu ungeondoka pale na ile furaha yetu ya kumtandika mtu katika nchi ile na kushinda ile mechi ingekuwa vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo hata wakati wa kurudi usumbufu ulikuwa vile vile. Kwa hiyo, naridhia na nawaomba Waheshimiwa Wabunge turidhie jambo hili kwa sababu faida ni nyingi kuliko hasara. Ukiona uwekezaji mkubwa ambao Serikali ya Chama cha Mapinduzi inawekeza sasa hivi katika kununua ndege na juzi tu tumepata ndege ya kusafirisha mizigo, tukiongeza *network* ya mashirikiano itatusaidia sana kuhakikisha kwamba ndege yetu inapeleka mazao sehemu nyingi sana na inaongeza wigo ndani ya nchi na katika nchi zingine za Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku moja Mheshimiwa Bashe anaweza akaelekeza ndege ikatua pale Ifakara ikachukua mchele, ikapeleka katika Nchi za Afrika hizo zitakazokuwa zimesaini kama ni 55 ama ni vipi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa suala la ajira; kuna watu wamekuja kusaidia Shirika letu la Ndege la Tanzania kutokana na

uzoefu wao katika mahusiano ya umoja wa mashirikiano ya anga katika nchi nyingine. Tutamkumbuka vizuri sana marehemu Mheshimiwa Omary Nondo, Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema, alitolewa katika mashirika haya ya kimataifa ya mashirikiano haya yaliyopita na akaja kutoa uzoefu mkubwa sana katika nchi yetu. Pia, tuna mifano mingi ya Nchi nyingine kama vile Misri, wanajiunga na hii Katiba ya Afrika lakini wanajiunga na Umoja wa Nchi za Kiarabu. Yote hii ni kuongeza *network* ya biashara katika safari ya anga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niseme kwa kifupi kwamba, pamoja na mambo yote aliyoyasema ya mafanikio kwa mfano ya kupata miongozo ya ndege ya kutosha. Sisi sasa hivi tunaongeza ndege nne, nafikiri kwenye Kamati yetu tumepewa. Kama tunaongeza ndege nne halafu tunajifungia wenyewe kwenye *East Africa* na Nchi kama Tanzania, bado hatuna soko kubwa la kujiwekeza vya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naijua tahadhali ambayo imesemwa na baadhi ya watu kwamba lazima tuweke kanuni au utaratibu mzuri tusije tukafungua anga tu halafu ikawa kama tunafungua soko la watu wengine. Hata hivyo, katika soko kubwa hilo hilo na sisi tunaweza kufanya vizuri zaidi kwa kuuza ndege zetu, kuuza Kiswahili chetu, kupambania vijana kupata ajira katika shirika hilo na katika nchi nyingine. Pia, sambamba na kupata fedha za uwekezaji ambazo zitatolewa na hiyo *AFCAC* ili nchi yetu iweze kufanya vizuri katika biashara ya usafiri wa anga.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kumalizia kwa kuwaomba Waheshimiwa Wabunge turidhie Mkataba huu, turidhie Katiba hii ya 2009 ili iweze kutumika na nchi yetu iingie katika *network* ya Afrika nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Kabla ya Mheshimiwa Innocent, Mheshimiwa Ally Jumbe Mlaghila, halafu atakuja Mheshimiwa Innocent na tutamalizia na Mheshimiwa Stella.

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia kulishawishi Bunge liridhie na kuunga mkono Katiba ya Tume hii ya *African Civil Aviation Commission.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania sio kisiwa, hatuwezi tukaishi kama kisiwa na tukajifanya na sisi tunao uwezo wa kuwa na mabavu tukiwa peke yetu. Lazima tuungane na Nchi Wanachama wa *AU* (Umoja wa Afrika) ambao wameridhia pamoja na Tanzania kwenye Katiba ya Tume hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, *industry* ya usafiri wa anga kwa sasa inakua sana. Vile vile, Tanzania tumeanza kuingia huko kwa nguvu kubwa sana. Tunapokwenda kwa nguvu ni lazima tujue na tuungane na wenzetu ambao wako kwenye *industry* hiyo ili twende tukapate uzoefu na manufaa makubwa ambayo yanatokana na usafiri wa anga.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa nini turidhie? Kwanza, tayari nchi nyingine zimekwisharidhia. Pili, hivi tunavyoongea Tanzania inalipa ada bila kuridhia. Tunalipa ada ambayo haitakuwa na manufaa, lakini tukiwa tunalipa ada tukapa manufaa itasaidia zaidi. Hivi tunavyoongea mpaka mwaka 2023 Tanzania imekwishalipa dola 45,230 karibu milioni 108. Hizi pesa hatuwezi tukakubali ziende bure. Kwa maana hiyo, naomba na nilishawishi Bunge twende huko turidhie Katiba hii ambayo itakuwa ni silaha kubwa ya sisi kujinufaisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakwenda kupata ajira kwa vijana wetu, tunakwenda kupata ajira kwa watu wetu kuingia kwenye eneo hilo, lakini pia tutafaidika na Sheria nyingi na mabadiliko yanayotokea ya *ICAO*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukikaa huko ndani, tuna fursa kubwa ya kueneza lugha yetu ya Kiswahili na tutaweza kutumia fursa zote zinazopatikana ili kuwafanya wenzetu waone umuhimu wa Kiswahili ambacho tunakitumia kama lugha bora kabisa na ambayo inashika nafasi kubwa Afrika na duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Watanzania tumelelewa vizuri sana na Baba wa Taifa. Vile vile, Baba wa Taifa alikuwepo kwenye kuanzisha Umoja wa Afrika *(OAU)* mwaka 1963. Tulipoanzisha Umoja wa Afrika *(AU)* ndipo mabadiliko yalipotokea. Pia huko nyuma tulikuwepo na tulikuwa tumeunga mkono Katiba ya Umoja huu. Baada ya mabadiliko mwaka 2009, ndipo tulipokuwa nyuma. sasa niliombe Bunge hili tuungane kwa pamoja turidhie na sisi tuangalie faida tunazozipata ambazo ni kubwa na ni nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Innocent, jiandae Mheshimiwa Stella.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyoko mbele yetu ya kuridhia Tume ya Katiba ya Usafiri wa Anga Afrika ya 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kuleta Azimio hili ndani ya Bunge lako tukufu. Kubwa zaidi niseme neno moja tu kwamba naunga mkono azimio hilo lakini naunga mkono maazimio na ushauri uliotolewa na Kamati ya Miundombinu kwa Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama walivyotangulia kusema wachangiaji waliotangulia, kwa kweli tumechelewa na katika kuchelewa kwetu naamini kabisa yako mambo mengine mazuri ambayo tumeyakosa sisi kama nchi kwa kuchelewa kujiunga na Tume hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie faida. Mojawapo ya faida kubwa ni kwamba, kama nchi tutakuwa katika mawasiliano ya uhakika ya usafiri wa anga na usalama wa anga letu kwa kujiunga na Tume hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kama nchi tutakuwa tunapata faida kwa kupata teknolojia mpya za ulinzi na usalama wa anga letu kwa kujiunga na Tume hiyo kwa sababu moja. Kama Nchi Wanachama kuna fursa nyingi za mafunzo zitakuwa zinatolewa kwa ajili ya ulinzi wa anga letu. Kwa hiyo, sisi kama nchi tunaamini kabisa tutakuwa tumepata msaada huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyosema ndugu yangu Mheshimiwa Mlaghila kwamba, kama nchi kupitia Tume hiyo tutakwenda kukuza Kiswahili chetu. Vijana wetu wataweza kupata ajira katika nchi hizo ambazo ni wanachama wa Tume hiyo na tutakuwa tumekuza lugha yetu ya Kiswahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, hapa tumeelezwa kwamba *CAG* ndiye Mkaguzi Mkuu wa Tume hiyo ya usafiri wa anga wa Afrika. Kwa hiyo, kwa namna moja au nyingine kama nchi tumepata heshima kubwa sana ya kwamba *CAG* wetu ameweza kutambulika katika Afrika na kwenda kukagua Tume kubwa ya Anga. Tuna kila sababu ya kukubaliana na hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika faida hizo pia nizungumzie hasara. Ni kweli kwamba tunazungumza kwamba tunapofungua anga Shirika letu la Ndege linaweza likamezwa, lakini naamini kwamba kadri tunavyokuwa tunakwenda, tutakuwa tunazidi kujipanua vizuri na tutalisaidia shirika letu, kwa sababu shirika letu pia linatakiwa litoke nje ya nchi na likafanye kazi katika nchi nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutokujisajili wenzangu Wanayanga waliokwenda kule Algeria, walipata matatizo makubwa...

**NAIBU SPIKA:** Hivi hakuna mifano mingine mpaka huo tu? *(Kicheko)*

**MHE, INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, unajua Simba wasingepata shida hiyo kwa ajili ya uzoefu wa mechi za Kimataifa, lakini Wanayanga walipata shida kubwa sana, *almost three hours* walibaki pale uwanjani nchini Algeria wakifuatilia taratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niombe tu kwamba tusije tukaingia katika shida nyingine za hapa na pale na nyingine kama hizo. Turidhie na niwaombe na niwashawishi Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba jambo hili ni jepesi wala halina mashaka yoyote. Faida ni kubwa kuliko hasara ambazo tunajaribu kuzionesha. Niwaombe na nishauri Bunge lako turidhie na tuingie katika Mkataba huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Stella, jiandae Mheshimiwa Naibu Waziri.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia katika Katiba ya Usafiri wa Anga Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kusema naunga mkono azimio hili kutokana na umuhimu wake. Pamoja na kuunga mkono nina mambo machache ya kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukubaliana kwa azimio hili ni kwamba tumekubali kuingia katika ushirikiano na ushindani wa kibiashara. Hata hivyo, kama tumekubali kuingia katika suala zima la ushindani wa kibiashara ni lazima tuangalie shirika letu. Je, lina uwezo wa kukabiliana na huo ushindani ambao tunakwenda kuingia?

Mheshimiwa Naibu Spika, ukirudi kwenye hali halisi ya shirika letu la usafirishaji limekuwa likikabiliana na changamoto nyngi sana. Vile vile, tumeona katika taarifa mbalimbali ikiwemo taarifa ya *CAG* namna ambavyo shirika hili limekuwa likikabiliana na matatizo makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa kuwa tunakwenda kuingia kwenye ushindani wa kibiashara ni lazima Serikali ikubali kufanya mabadiliko kwenye suala zima la ushindani wa kibiashara ili twende tukafaulu kwenye suala zima la ushindani wa kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona kabisa kwenye taarifa ya *CAG* namna ambavyo shirika limepata hasara kwa miaka mitano mfululizo. Sasa kama tunakwenda kuingia kwenye ushindani wa kibiashara na tunaona kuna maeneo ambayo shirika letu linakwama, ni lazima tuwe na mambo ya kushauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia taarifa ya *CAG* hiyo hiyo ya mwaka 2022, inasema wazi kabisa kwenye suala la ukaguzi wa mashirika ya umma namna ambavyo shirika lina madeni makubwa kuliko mtaji lilionao. Sasa, kama tunakwenda kuingia kwenye ushindani wa kibiashara ni lazima Serikali ikubali kuyatazama haya ili tusiende kuaibika huko mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya *CAG* inasema wazi kabisa kwamba mtaji ambao shirika lilikuwa nao ni bilioni 295.2, wakati huo madeni ambayo shirika linadaiwa ni bilioni 535. Tafsiri yake shirika lina mtaji hasi…. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Stella, changia hoja ambayo iko mbele yako. Changia mjadala wa kuridhia kuingia katika huu Mkataba wa *Civil Aviation.*

**MHE. STELLA S. FIYAO:** *(Hapa alizungumza bila kutumia kipaza sauti)*.

**NAIBU SPIKA:** Wewe hebu kaa kimya. Mimi naongea na wewe unasema, kama nani? Kuna shirika gani katika dunia sasa hivi linatengeneza faida kwenye ndege? Nitajie moja tu. Changia hoja iliyokuwepo mbele, kama umemaliza kaa chini. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Naibu Spika ni lazima tutoe angalizo kama Bunge. Ni vema Serikali ikajidhatiti katika kuwekeza kwenye shirika hili ili tupate matokeo yaliyo sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza, naomba kuishauri Serikali iwekeze kwenye shirika hili ili liweze kujiendesha kibiashara. Jambo la pili, Serikali iwekeze kwenye shirika hili ili tuweze kuinuka kidedea katika suala zima la ushindani wa kibiashara. Hatuwezi kuingia kwenye ushindani wa kibiasharra kama Serikali haijakubali kuwekeza kwa asilimia mia moja kwenye shirika hili, tuta-*fail* na tutaaibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka kushauri, kumekuwa na changamoto nyingi za ukamataji wa ndege. Ni vema Serikali ipitie kesi za madai za kitaifa ili kuepusha changamoto ya ukamataji wa ndege na kuziingiza ndege zetu kwenye hatari ya kukamatwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kusema hayo naunga mkono Azimio, lakini naomba Serikali iyazingatie niliyoshauri. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri nafasi yake atamalizia Waziri mwenyewe. Mheshimiwa Waziri, mtoa hoja.

*(Hapa Naibu Waziri wa Uchukuzi Mhe. Atupele F. Mwakibete alisimama kwa ajili ya kutaka kuchangia)*

**NAIBU SPIKA:** Ulishatoa taarifa kwangu ume-*withdraw* na ukitaka kuchangia tena lazima uniambie unachangia tena. Mheshimiwa Waziri, sasa mwache aendelee Naibu Waziri. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ili niweze kuchangia kuhusu kuridhia Azimio hili la *AFCAC*. Naungana na Mheshimiwa Waziri pamoja na Kamati kwa namna ambavyo wameweza kuwasilisha jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili lina faida kubwa sana kwa nchi yetu, mpaka sasa tumechelewa. Kama ambavyo amesema Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake kwamba nchi zaidi ya 15 zimekwisharidhia, lakini sisi kama nchi bado hatujaridhia. Kuna faida kubwa sana kwa Taifa letu. Waheshimiwa Wabunge wengi hapa wameelezea faida ambazo zinatokana na kuridhiwa kwa itifaki hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba Waheshimiwa Wabunge waweze kuridhia jambo hili. Faida zake zimeelezwa kinagaubaga ikiwemo suala la kukuza lugha yetu ya Kiswahili, katika Katiba limeelezewa vizuri kabisa. Ukiisoma Katiba yetu kuanzia *Article* 24 imeeleza lugha itakayotumika ni pamoja na Kiswahili. Kwa hiyo, tutakuwa na sifa muhimu kwa ajili ya kueneza lugha yetu ya Kiswahili kwa Bara zima la Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni pamoja na soko shindani. Mheshimiwa Stella Fiyao amesema hapa, kwamba tujipange kama Serikali. Nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba kama Serikali tumejipanga vizuri kwa ajili ya kushindana na ndio maana na sisi kama nchi tunahitaji kuridhia ili tuendane na ulimwengu wa kileo. Kama tuliridhia mwaka 1969 na Katiba mpya ya 2009 tulisaini tangu mwaka 2010. Tulikuwa hatujaridhia kwa kipindi chote hicho tukisubiri wenzetu waweze kuridhia. Sasa nchi zaidi ya 15 zimeshasaini, maana yake sasa hivi sisi tuko nje ya mfumo ama hatuko ndani ya itifaki hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Watanzania wote kwamba kama Serikali tumejipanga vizuri katika soko hili shindani na hata ndege ambazo Mheshimiwa Rais amekuwa akitoa fedha kwa ajili ya kununua haziwezi kufanya kazi Tanzania peke yake. Tunahitaji kwenda kwenye mabara mengine, ili tukienda huko watalii waweze kuja lakini pia tufanye biashara na mataifa mengine. Hatuwezi kufanya hivyo kama jambo hili tutakuwa hatujaliridhia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini sio kwa umuhimu, Mheshimiwa Dkt. Chamuriho pia alizungumza suala la ni namna gani tumejipanga kutokana na mkataba ambao ulisainiwa kule Senegal Yamoussoukro. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tumejipanga kwa namna hii; kwanza, kuna mikataba kati ya nchi na nchi lakini pili kuna mikataba kati ya bara na bara. Kwa namna sisi tunavyofanya mpaka sasa tutatumia mkataba unaoitwa *BASA* yaani *Bilateral Air Services Agreement*. Hata sasa tunafanya hili, kwa hiyo tusiwe na mashaka kwamba pengine tukiridhia makampuni makubwa kama *Emirates* yanaweza kuja ndani ya nchi, halafu yakaanza kufanya *shunting* za ndege kwa mfano kutoka Dar es Salaam kwenda mikoani, hilo halitakuwa hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa mtoa hoja.

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijafanya hitimisho la hoja iliyoko mbele, naomba kufanya masahihisho kidogo tu. Wakati natoa hoja yangu nilisema Mkutano wa Kumi na Moja, lakini huu ni Mkutano wa Kumi na Mbili, naomba isomeke hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote tena, napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana hapa kwenye Bunge letu Tukufu na kujadili hoja hii iliyo muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kukushukuru wewe binafsi, kwa jinsi ulivyoongoza majadiliano kwenye hoja hii ya Katiba ya Tume ya Usafiri wa Anga wa Afrika ya Mwaka 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kipekee nimshukuru Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Mheshimiwa Selemani Moshi Kakoso pamoja na Waheshimiwa wote, Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu kwa jinsi ambavyo walichangia hoja hii na jinsi ambavyo walichambua hoja hii kwanza kuanzia kwenye Kamati mpaka walipokuja hapa Mwenyekiti amechangia vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiri kwamba hoja hii ni muhimu sana kwa maendeleo na ukuaji wa Sekta ya Anga hapa nchini. Pia, nawashukuru Waheshimiwa wote Wabunge waliochangia hoja hii, tumezichukua hoja zao na tunaenda kuzifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hoja za Kamati ya Bunge ya Kudumu zilikuwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ya kwanza ilikuwa ni kutoa fursa kwa lugha ya Kiswahili itangazwe. Pili, fursa za soko la ajira pamoja na za anga pia, wadau wengine washirikishwe. Yote haya tumeyachukua tunaenda kuyafanyia kazi, tutaboresha zaidi au tutaitangaza zaidi Lugha ya Kiswahili, pamoja tutatangaza zaidi soko la anga hapa Tanzania pamoja na kuwashirikisha wadau.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Chamuriho yeye ana wasiwasi tu ambao ameonyesha kuhusu Mkataba wa Yamoussoukro. Ukweli wenyewe kama alivyosema Naibu Waziri, kwamba mkataba wa nchi na nchi unaongozwa na *Bilateral Air Service Agreement*. Kwa mfano, leo Kenya wamesaini Katiba hii, Rwanda wamesaini Katiba hii, lakini Rwanda yeye haiwezi kutoka ikaenda Nairobi ikachukua abiria kupeleka Mombasa, haiwezi. Kwa sababu inaongozwa baina ya Kenya na Rwanda ni *Bi-Service*

*Agreement* au *Bilateral Service Agreement* baina ya Kenya na Rwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunayo na nchi mbalimbali, tuna na Kenya, tuna na Rwanda na nchi nyingine mbalimbali, tunayo mikataba hiyo. Hiyo ndio inaongoza utaratibu wa kutoa abiria kutoka eneo moja kwenda la pili. Leo kwa mfano, *KLM* inafika Kilimanjaro lakini haiwezi kuchukua abiria wa ndani kutoka *KIA* kuwaleta Dar es Salaam. Kwa hiyo, tumepokea maoni ya Mheshimiwa Dkt. Chamuriho, tunayaheshimu na tunaenda kuyafanyia kazi, lakini nimhakikishie tu kwamba usaifiri wa anga nchini upo salama na *Air* Tanzania tutaendelea kuilinda ili iweze kufanya kazi iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, sasa naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono. Waheshimiwa Wabunge sasa nitawahoji, kuhusu Bunge kukubali kuridhia Mapendekezo ya Katiba ya Tume ya Usafiri wa Anga ya Afrika ya Mwaka 2009 *(The Constitution of the African Civil Aviation Commission, 2009)*.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Mapendekezo ya Katiba ya Tume ya Usafiri wa Anga ya Afrika ya Mwaka 2009 (The Constitution of the African Civil Aviation Commission, 2009) yaliridhiwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, nikushukuru Mheshimiwa Waziri kwa ku-*present* vizuri na ni hoja za msingi na *concern* ya Mheshimiwa Dkt. Chamuriho, najua Mheshimiwa Dkt. Chamuriho ni mtaalam wa haya mambo, lakini *be assured* hivi vitu haviwezi kwenda bila Serikali kuvisimamia kwa

ukamilifu. Hatuwezi kubaki kama kisiwa lazima tucheze nao, huko huko walipo na sisi tucheze nao. Nina mfano mdogo kama kabla Simba isingejitutumua sasa hivi tungekuwa wapi? Imekwenda kupambana na ma-*giant* matokeo yake mnayaona sasa hivi. *(Makofi)*

Timu nyingi zime-*benefit* kutokana na mchango wa Klabu ya Simba na *Air* Tanzania vilevile itapata uzoefu na itapata mafanikio makubwa, leo *Emirates* imeungana na *Air Qantas* ya Canada. Kwa hiyo mashirika haya yameungana kwenye kutafuta pesa, kutafuta abiria. Kuna nchi ya jirani iliuza *route* yake ya alfajiri ya kwenda *London for 50 million Dollars*. Kwa hiyo, hivi vitu vya ndege vinataka kujua na tuna wataalam wazuri kwenye *civil aviation* ambao na wao wanajua ku-*scout* na kuwa na *market intelligence* kwenye *aviation*.

Waheshimiwa Wabunge, *aviation* sio biashara tu, biashara hii inahitaji wataalam sana ambao sisi Tanzania tunao. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri hongera sana kwa Azimio hili na tunawatakia kila la kheri, lakini tahadhari zilizotolewa zichukuliwe na mzifanyie kazi na wataalam waanze kuhakikisha kuwa maslahi mapana ya Taifa yanapatikana.

Baada ya maneno hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 5.43 Asubuhi Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 31 Agosti, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*